# HAZINA YETU

## TOLEO LA PILI MWAKA 2024/25



# KUTOKA MEZA YA KATIBU MKUU



**Ndugu Wasomaji,**

Nina furaha kubwa kuwakaribisha kwenye Toleo hili la Pili la Jarida la Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25, linalotumika kama moja ya nyenzo ya Mawasiliano ya Kimkakati ya Wizara yetu kwa ajili ya kufikisha Taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukumu yetu, ikiwemo Sera, Programu na Matukio mbalimbali.

Ninachukua fursa hii kuwafahamisha kuwa Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, Tanzania imeendelea kuchukua hatua thabiti za kuimarisha uchumi, kuhakikisha usimamizi bora wa fedha za umma, na kukuza maendeleo jumuishi kwa ustawi wa Taifa letu.

Kwa ujumla, uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara licha ya changamoto za kiuchumi zinazoshuhudiwa duniani. Tumeshuhudia ongezeko la mapato ya ndani kutokana na maboresho ya usimamizi wa kodi na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika ukusanyaji wa mapato. Pia, mageuzi katika sekta ya fedha na uwekezaji yamechangia kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza imani kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Katika sekta ya matumizi ya serikali, tumesisitiza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma, kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa tija.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, ikiwemo uboreshaji wa miundombinu, na huduma za kijamii kama kilimo, maji, elimu na afya.

Katika masuala ya kimataifa, ushiriki wa Tanzania katika Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia umeendelea kuimarisha ushirikiano wetu na Taasisi hizo za kifedha duniani, jambo linalosaidia katika upatikanaji wa rasilimali kwa maendeleo ya taifa.

Tunapoendelea na mwaka wa fedha 2024/25, tunahimiza wadau wote kushirikiana kwa karibu katika kujenga uchumi imara, endelevu, na jumuishi. Tutaendelea kuboresha sera za kifedha, kusimamia matumizi ya Serikali kwa ufanisi, na kuweka mazingira mazuri kwa ukuaji wa sekta binafsi.

Nakutakia usomaji mwema wa jarida hili, na naomba tuendelee kushirikiana katika kuhakikisha mafanikio ya kiuchumi ya nchi yetu ikiwemo kulipa kodi kwa hiari, kudai risiti na kutoa risiti tunapouza au kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali.

**Dkt. Natu El-maamry Mwamba**
Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha

# NENO LA MHARIRI MKUU



**Ndugu Wasomaji,**

Karibuni mjisomee Jarida la Hazina Yetu la Robo ya Pili ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, kuanzia Mwezi Septemba hadi Desemba, 2024, tunalolitoa katika mfumo wa nakala laini na nakala ngumu, na kuandaliwa na kuzalishwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha.

Kwenye toleo hili tunawaletea Makala mbalimbali na taarifa muhimu na za kina kuhusu Elimu ya Fedha inayotolewa na Serikali kupitia Wizara yetu na Taasisi zake kwa wananchi ili kuongeza uelewa wa masuala ya kifedha na kukuza ushiriki wa kila mmoja katika uchumi rasmi. Pia, tunaangazia sekta ya Ununuzi na Ugavi, ikiwa ni mhimili muhimu wa usimamizi wa rasilimali za umma kwa uwazi na ufanisi.

Mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuwa mada muhimu duniani, na hivyo tunawaletea uchambuzi wa Ufadhili wa Mapambano dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi ili kuonyesha hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo pamoja na mijadala ya kimataifa kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na njia za kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabianchi. Zaidi ya hayo, tunakuletea muhtasari wa vikao vya Bunge, taarifa kuhusu matukio muhimu ya Mikutano ya Mwaka ya Taasisi za Fedha Duniani, ikiwemo Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia, iliyofanyika 2024, Washington D.C, Marekani.

Nawatakia usomaji mwema.

**Benny Mwaipaja**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha



# Makala

# IFAHAMU WIZARA YA FEDHA

*Na. Eva Ngowi*

Katika makala iliyopita ya Ifahamu Wizara ya Fedha, tuliangazia historia fupi ya mabadiliko ya Jina la Wizara pamoja na uongozi wa Mawaziri wa Fedha baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na kuanza kutekeleza majukumu yake rasmi mwaka 1962.

Mabadiliko hayo yalilenga kuboresha ufanisi, uwazi, na uwajibikaji katika utawala wa fedha za umma, huku lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinatumika kwa manufaa ya wananchi wote.

Katika kipindi cha miongo kadhaa tangu uhuru, Wizara ya Fedha imekuwa na mchango mkubwa katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa, ikiwa ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa sera za maendeleo ya Taifa.

Katika mwendelezo wa makala yetu, tutajikita kwa undani zaidi katika majukumu makuu yanayotekelezwa na Wizara ya Fedha, na jinsi yanavyogawanywa kulingana na Idara na Vitengo vilivyopo ndani ya Wizara hii.

Wizara ya Fedha, kama ilivyoainishwa katika makala yetu iliyopita, inajumuisha Idara 13 na vitengo 6, ambapo kila moja ya Idara na Vitengo hivi ina majukumu yake maalumu, yanayotekelezwa




kila siku kwa mujibu wa miongozo, sera, na mikakati ya Serikali. Majukumu haya ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Serikali inafanya kazi kwa ufanisi na kwa uwazi, huku ikiwezesha maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi.

Katika makala haya, tutazungumzia kwa kina Idara mbili za kwanza za Wizara ya Fedha. Idara hizi ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya wizara, na kila moja inahusika na masuala muhimu ya kifedha, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa matumizi, na utekelezaji wa sera za kifedha za Taifa. Katika makala haya tutatoa mwanga wa kina kuhusu kazi za kila Idara, na michango yake katika kuleta maendeleo ya Taifa.

## Idara ya Uchambuzi wa Sera

Idara hii ina sehemu tatu kuu ambazo kila moja ina jukumu maalum katika kuboresha hali ya Uchumi na kifedha.



**Dkt. Johnson J. Nyella**

Kamishna wa Idara ya Uchambuzi wa Sera

**1** **Sehemu ya kwanza ni Sehemu ya Sera za Fedha, inayoshughulikia upangaji, uchambuzi na utekelezaji wa sera za fedha.**

Inahusisha usimamizi wa bajeti za Serikali, upangaji wa kodi na matumizi ya umma. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba sera za fedha zinaendana na malengo ya kiuchumi ya Serikali, na hivyo kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

**2** **Sehemu ya pili ni sehemu ya Sera za Uchumi Mpana (Macro-economics). Sehemu hii inalenga katika sera zinazohusu Hali ya Uchumi Jumla.**

Hii inajumuisha udhibiti wa mfumuko wa bei, mikakati ya kupambana na ukosefu wa ajira, na ukuaji wa uchumi. Wataalamu wa sehemu hii wanafanya kazi kuhakikisha kwamba sera zinazotekelezwa zina madhara chanya kwa uchumi wa Taifa na kwamba zinahimiza ukuaji endelevu.

**3** **Sehemu ya tatu ni sehemu ya Utafiti na Uundaji wa Miundombinu ya Kifedha.**

Sehemu hii inajishughulisha na tafiti za kina na uundaji wa mifumo ya kifedha ili kutoa makisio sahihi ya mwenendo wa kiuchumi. Wataalamu wa sehemu hii wanachambua data za kifedha, kutengeneza mifumo ya utabiri, na kusaidia katika kufanya maamuzi yenye taarifa sahihi. Matokeo ya tafiti zao yanasaidia katika kuunda sera bora na kuimarisha mipango ya kiuchumi.

Kwa pamoja, Sehemu hizi tatu zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha sera za kiuchumi na kufanikisha malengo ya maendeleo ya Taifa. Kila Sehemu ina jukumu lake maalum lakini zote zinashirikiana ili kuhakikisha kuwa sera zinazotekelezwa zinakuwa na matokeo chanya katika uchumi.

## Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali:

Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali ilianzishwa rasmi mwezi Disemba, 2019, ambapo kabla ilikuwa kitengo ndani ya Idara ya Uchambuzi wa Sera.

Idara hii imepewa jukumu la kusimamia deni la Serikali na kuhakikisha Serikali inapata fedha zenye masharti nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na ile ya kimkakati, cbila kuathiri uimara wa deni la Serikali; na kupunguza hatari zinazohusiana na deni kwa kiwango kinachokubalika.



**Bw. Japhet Justine**

Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali

Katika kutafuta mikopo ya nje na ya ndani, Idara ya Usimamizi wa Madeni (DMD) inaongozwa na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134 (GLGGA); Mkakati wa kati wa muda wa kati wa usimamizi wa madeni (MTDS) na Mwongozo wa Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na Misaada.

Idara ipo chini ya fungu Na. 21 na imegawanyika katika vitengo vitatu ambavyo ni:

i. Kitengo cha Utafutaji wa Fedha 'Debt Resource Mobilization Section' kinachoongozwa na Kamishna Msaidizi;

ii. Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi vya Madeni 'Debt Risk Management Section' kinachoongwa na Kamishna Msaidizi;

iii. Kitengo cha Usimamizi wa Kanzidata ya Madeni 'Debt Database Management Section' kinachoongozwa na Kamishna Msaidizi. Aidha, Idara pia ina kitengo cha Uhasibu kinachosimamia masuala ya malipo na uhasibu

**1** **Kitengo cha Utafutaji wa Fedha**

Kitengo hichi kinajishughulisha na *Moja,* Kutafuta fedha za kuziba nakisi ya bajeti kutoka vyanzo vya kibiashara nje na ndani ya nchi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. *Pili,* Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Ukopaji katika Soko la Ndani (Domestic Borrowing Plan) na kuendeleza soko la dhamana za Serikali (Domestic Bond Market Development) kila mwaka.

*Tatu;*kuendelea kuweka mazingira mazuri katika soko la upili ili kuongeza uwekezaji katika soko la awali ambapo wawekezaji wanakuwa na uhakika kwa kuuza dhamana hizo. *Nne;* Kufanya Tathmini ya Nchi Kukopesheka katika Masoko ya Kimataifa (Sovereign Credit Rating).

## 2 Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi vya Madeni

Kitengo hichi kinafanya majukumu kama; *Moja*, Kuratibu vikao vya kamati za usimamizi wa madeni, Technical Debt Management Committee (TDMC) na National Debt Management Committee (NDMC). *Pili;* kuchambua maombi ya mikopo, dhamana na misaada kutoka Wizara, Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali inayolenga kutekeleza miradi ya maendeleo na kuwasilisha kwenye kamati hizo. *Tatu;* Kuandaa, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Muda wa Kati wa Usimamizi wa Madeni (Medium Term Debt Management Strategy -MTDS). Aidha, Mkakati unaelekeza kwamba mikopo yote ya kibiashara ielekezwe kwenye miradi ya kimkakati inayochochoea ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi. *Nne;* Kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali (Debt Sustainability Analysis-DSA) kila mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

## 3 Kitengo cha Usimamizi wa Kanzidata ya Madeni

Kitengo hichi kinafanya majukumu kama; *Moja;* Kusimamia kanzidata ya madeni ya Serikali pamoja na kurekodi mikopo na kuandaa malipo ya madeni yanayoiva. *Pili;* Kuandaa ripoti za robo mwaka za mwenendo wa deni la Serikali. *Tatu;* Kufuatilia na kusimamia madeni sanjari, yaani madeni yaliyotokana na dhamana za Serikali (management of contingent liabilities) kwa nia ya kuhakikisha madeni haya hayaathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali. *Nne;* Kuratibu ulipaji wa Deni la Serikali kupitia fungu 001. *Tano,* Kusimamia utekelezaji na maboresho ya Sheria ya Mikopo, dhamana na Misaada Sura 134 na Kanuni zake. *Sita;* Kusimamia na kutoe Elimu kuhusu mwongozo wa Miradi na majadiliano ya Mikopo, dhamana na Misaada. *Saba;* Kushiriki kwenye majadiliano (Bilaterals) ya Msamaha wa madeni na Nchi za kundi lisilo wanachama wa Paris-Club. *Nane;* Kuratibu matumizi ya Fedha za Debt Swap kati ya Tanzania na Spain kupitia miradi itakayoibuliwa na Nchi mbili.

## VIPAUMBELE VYA IDARA YA USIMAMIZI WA DENI LA SERIKALI

i. Kulipa riba na mtaji wa deni la ndani na nje la Serikali kwa usahihi na kwa wakati pindi linapoiva.

ii. Kuendelea kufanya mapitio ya Tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni baada ya nchi kutathimiwa na kutunukiwa alama B1 na B+ na Moody's Investors Service Ltd na Fitch Rating Services Ltd mtawalia.

iii. Kusimamia deni la Serikali kuhakikisha linaendelea kuwa himilivu katika muda wa kati na mrefu ambapo viashiria vya deni vimeendelea kuwa ndani ya wigo unaokubalika.

iv. Kutafuta fedha za mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje vyenye masharti ya kibiashara (non-concessional loan) ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na ile ya kimkakati.

v. Kusimamia na kutunza kanzi data ya Madeni.

***Itaendelea ...***

# JUKWAA LA WADAU WA SEKTA YA FEDHA MAPINDUZI YA UKUAJI WA UCHUMI WA NCHI

*Na. Farida Ramadhan*

Sekta ya Fedha ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Nchi na kupunguza umaskini.

Ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi kwa kuwa inahakikisha uwepo wa mifumo rasmi ya kifedha inayowezesha uwekezaji, biashara na maendeleo ya kijamii.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta hiyo katika uchumi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kisera na kisheria ili kuboresha utendaji na ufanisi wa sekta hiyo ikiwemo kuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kwa mwaka 2020/2021-2029/2030.

Mpango huo unalenga kuongeza upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha, upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu, kulinda watumiaji wa huduma za fedha, kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha, kujenga uwezo wa wadau wa sekta ya fedha, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika sekta ya fedha, kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu na kuweka mazingira wezeshi ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika sekta hiyo muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Katika hatua ya utekelezaji wa Mpango huo, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wa wa Sekta ya Fedha nchini ilianda Jukwaa la Kwanza la Wadau wa Sekta ya Fedha lililofanyika Desemba, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City jijini Dar es Salaam, kwa ajili kujadili fursa na hatua mbalimbali za kuboresha, kukuza na kuimarisha sekta hiyo muhimu nchini.

Jukwaa hilo linalenga kukuza na kuimarisha Sekta ya Fedha nchini kwa kushirikishana namna bora ya kukuza matumizi ya teknolojia na uvumbuzi pamoja na kuufahamisha Umma hatua mbalimbali za maboresho ya Kisera na kisheria yaliyofanyika ikiwemo ujumuishaji wa huduma za kifedha, uendelevu wa huduma za kifedha na huduma za fedha kwa njia ya kidigitali.

Akifungua Jukwaa hilo Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alisema kuwa Serikali itaendelea kuzichukulia hatua kali Taasisi zinazotoa mikopo yenye riba kubwa (mikopo kausha damu) ambayo imekuwa ikirudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi na kuwaongezea wananchi umasikini.

Dkt. Nchemba alisema taasisi hizo sio hatari kwa wananchi pekee bali ni hatari kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla kwa sababu zimekuwa zikiwaumiza wananchi kwa kutoa mikopo yenye riba kubwa, kuwadhalilisha pamoja na kuwadhulumu kwa kupanga njama za kuwafilisi wale ambao wanajua wazi hawataweza kulipa mikopo hiyo.





*Tutaendelea kuchukua hatua kali kwa wale wote wanaofanya shughuli za kausha damu, na popote Mtanzania ukiona hiyo shughuli inafanyika fichueni taarifa hizo ili tuweze kukomesha utaratibu huo wa kinyonyaji", alisistiza Mhe. Dkt. Nchemba.*



Aidha, Dkt. Nchemba alitoa maagizo kadhaa kwa wadau wa Sekta ya Fedha nchini ili kuimarisha sekta hiyo muhimu katika kukuza uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Aliwaagiza wadau hao kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa wananchi ili wajue kutofautisha kati ya Taasisi rasmi na zisizo rasmi, kwa kuonesha faida na usalama wa taasisi rasmi pamoja na hatari ya taasisi zisizo rasmi ambazo zinazotoa mikopo umiza.

*Nalisistiza hili na nitaendelea kusisitiza, lazima watu wetu watofautishe na waone kwamba kutumia urafiki, taasisi bubu ambazo hazijasajiliwa kama ndio tegemeo lao la kukopa ni jambo la hatari sana na si kwao tu hao wakopaji bali ni hatari pia kwa Taifa letu", aliongeza Mhe. Nchemba.*

Alisema wananchi wanatakiwa kuendelea kusisitizwa kuwa fedha za mkopo zisitumike kwa matumizi ya kawaida, zinatakiwa zitumike katika shughuli za uzalishaji ili kuweza kurejesha mkopo na kubainisha kuwa hata nchi haijawahi kukopa kwa ajili ya kulipa mishahara, ikikopa inapeleka fedha kwenye miradi mahusi ya maendeleo, kwa sababu miradi hiyo inaweza kuzalisha na kulipa deni.

Dkt. Nchemba aliwaagiza wadau wa Sekta ya Fedha kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), waongeze nguvu ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia benki kupata mikopo pamoja na kutunza fedha zao kwa kuwa kutunza fedha benki ni utaratibu wa kisasa wa uendeshaji wa uchumi.

Alisema wananchi waelimishwe na kuhakikishiwa kuwa kuweka fedha benki ni salama kwa sababu hivi sasa TRA inatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kukusanya kodi kwa weledi na kufuata Sheria kwa kutofunga akaunti za wateja wanaowadai kodi.

Aliwaagiza viongozi wa Taasisi za Fedha nchini hususan benki kuhakikisha wanajiridhisha na kupata taarifa za kina kabla ya kuruhusu watumishi na madalali wao kupiga mnada mali zilizowekwa kama dhamana na wateja wao waodaiwa mikopo kwa sababu kuna baadhi ya watumishi wasio waaminifu hushirikiana na watu wengine kudhulumu mali hizo kwa njia ya mnada.

*Yanapotokea mambo ya mnada, viongozi wetu mjiridhishe kwanza, msikimbilie tu kutoa sifa kwamba tumekuwa wakali kurecover, halafu kumbe mmebariki deals za watu, kwa maana kwamba akatokea mteja akawa ameipenda dhamana iliyowekwa na mkopaji akahamasisha mteja alazimishwe kulipa au dhamana ipigwe mnada huku akijua dhahiri kwa shughuli anazofanya mkopaji hawezi kulipa deni lake kwa haraka, kumbe suala sio kurecover mkopo ni kupata dhamana ili iende kwa mtu mwingine", alibainisha Mhe. Dkt. Nchemba.*

*Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukusanya kodi kwa weledi unaozingatia sheria, bado hatuja wasiliana vizuri kuhusu msimamo huo, kuna baadhi ya maeneo bado wananchi wanaogopa kuweka fedha benki, nyinyi muwahakikishie kuwa kuweka fedha benki ni salama" alibainisha Dk. Nchemba.*

Alisema suala hilo ni la kupigwa vita kwa kuwa halina afya kwenye Sekta ya Fedha na sio utaratibu mzuri kwenye ustawi wa jamii na kufafanua kuwa minada mingi inawatia umaskini wananchi kwa sababu kuna wateja ambao wanakuwa wameshalipa mikopo yao kwa asilimia 80 halafu mali zao zinapigwa mnada kwasababu ya asilimia 20 tu.

Mhe. Dkt. Nchemba, pia aliwataka kuwa makini na suala la mikopo chechefu kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo watumishi wa Taasisi za Fedha nchini na wateja wasio waaminifu hupanga njama za kutengeneza mikopo chechefu.

Alisema mikopo mingi chechefu ikiangaliwa kwa unandani inaonesha wazi kuwa kuna watumishi wa benki wamehusika katika kuitengeneza mikopo hiyo tangu siku ambayo inatoka.

Hakuishia kwa wadau wa Sekta ya Fedha pekee, Mhe. Nchemba alitoa onyo kali kwa wananchi wote ambao wamekuwa wakiacha kulipa mikopo kwa makusudi huku wakikimbilia mahakamani kwa kudhani kuwa itachukua muda mrefu kutoa hukumu.

Alisema kwasasa Serikali imeshaamua kuwa masuala yote yanayohusu uchumi na kodi yatakayofikishwa mahakamani hayatachukua muda mrefu kuamuliwa, hivyo kuacha kulipa mikopo na kodi kwa makusudi na kukimbilia mahakamani hakutowasaidia chochote zaidi ya kujisogeza karibu na mikono ya sheria ambayo itawachukulia hatua kali.

Jukwaa la Wadau wa Sekta ya Fedha nchini ni mwendelezo wa juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali za kuhakikisha inaboresha na kuendeleza Sekta ya Fedha nchini na kutimiza lengo la kuhakikisha asilimia 80 ya wananchi wanafikiwa na elimu ya fedha ifikapo mwaka 2025.




*Waziri wa Fedha, Mhe, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (wa tatu kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (watatu kulia), Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bi. Sauda Msemo (wapili kulia), Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja (wa kwanza kulia), Mkurugenzi anayesimamia sekta ya hifadhi ya jamii ofisi ya waziri mkuu kazi, vijana, ajira na watu wenye ulemavu, Bw. Festo Fute (wa kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mkuu Benki ya NBC, Bw. Theobald Sabi, wakionesha nyaraka zilizoandaliwa za Sekta ya Fedha ambazo ni Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa Mwaka 2023/24 – 2028/29, Mwongozo wa Mitaji Halaiki (Crowd financing) pamoja na Mwongozo wa Utoaji Hati Fungani zinazozingatia Sharia kwa Kampuni na Taasisi za Umma wa Mwaka 2023 (Capital Markets*

# ELIMU YA FEDHA MSINGI WA MAENDELEO YA KIUCHUMI

*Na. Farida Ramadhan*

Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi", ni kaulimbiu ambayo imekuwa ikitumika kwa miaka miwili sasa katika Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa ambayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka.

Elimu hiyo ya Fedha ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Mwaka 2020/21 – 2029/30 ambapo Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Fedha nchini iliandaa Nyenzo ya Kufundishia Elimu ya Fedha inayoanisha maeneo muhimu ya kuzingatia wakati wa utoaji elimu ya fedha kwa umma.

Maeneo hayo ni pamoja na usimamizi wa fedha binafsi, uwekaji wa akiba, mikopo. uwekezaji, bima, bima ya amana, kodi, hatifungani pamoja na kujipanga na maisha ya uzeeni.

Elimu ya Fedha ni msingi wa maendeleo ya kiuchumi kwa sababu inawaezesha wananchi kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi bora ya kifedha kwa kupata uelewa wa jinsi ya kusimamia mapato na matumizi yao kwa ufanisi, kuwa na nidhamu ya matumizi sahihi ya fedha kupitia uwekezaji na uwekaji akiba katika mifumo rasmi.

Imekuwa ni mhimili muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi kwa sababu inapunguza umaskini na kuongeza kipato kwa kuwasaidia wananchi kuelewa fursa mbalimbali zinazopatikana katika Sekta ya Fedha na namna ya kuzitumia fursa hizo kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Inawawezesha wananchi kukabiliana na mikopo umiza ambayo imekuwa janga katika siku za hivi karibuni kwa kuwajengea uwezo wa kujua taasisi rasmi zinazotoa mikopo, malengo ya mikopo, riba, mikataba ya malipo ya mikopo pamoja na haki za mkopaji na mkopeshaji.

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Fedha nchini imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha wananchi wanafikiwa na elimu hiyo muhimu ambapo inalenga kuhakikisha elimu hiyo inawafikia asilimia 80 ya wananchi ifikapo mwaka 2025.

Pamoja na jitihada hizo bado kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Fedha, ambapo kwa kulitambua hilo kutokana na kutokuwa na msingi bora wa elimu ya fedha kwa wananchi, Serikali imeamua kuiweka elimu ya fedha rasmi katika mtaala wa elimu, ili kujenga msingi imara kwa wanafunzi kujua fursa zinazopatikana katika -



Kutokana na ukosefu wa elimu ya fedha, wananchi wengi wanakosa nidhamu ya fedha kwa kukopa bila malengo na kukosa fursa za kuboresha maisha yao kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi. Utafiti wa FinScope wa mwaka 2023, unaonesha kuwa ni asilimia 53.5 tu ya nguvu kazi nchini ndiyo wanaotumia huduma rasmi za fedha na hivyo kubaki na kundi kubwa la wananchi ambao hawafaidiki na huduma hizo.

Wahenga wanasema samaki mkunje angali mbichi, Serikali imeona ianze kutoa elimu ya fedha kwa wananchi tangu wakiwa wadogo ili kuwajengea msingi imara wa kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa maendeleo yao binafsi na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Pro. Adolf Mkenda alilibainisha hilo wakati akifungua Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, jijini Mbeya mwaka 2024, kwa kueleza kuwa kuanzia Januari, 2025 somo linalohusu masuala ya fedha, ujasiriamali na biashara kwa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne, litakuwa ni somo la lazima.




*Tumeliweka somo hilo ili kuwaanda wanafunzi wanapomaliza kidato cha nne wakiamua kuanzisha shughuli zao wenyewe wajue wanajipanga vipi, tunataka mtoto akimaliza kidato cha nne ajue fedha ni nini, akitaka kwenda benki anafanyaje, TIN namba ni nini, TRA ni nini na muhimu zaidi unawekaje taarifa zako lakini pia uwezekano wa kupata mtaji na kuendeleza ni muhimu zaidi", alibainisha Prof. Mkenda.*

Alisema Sekta ya Elimu imetengeneza mtaala huo ili kuunga mkono juhudi za Serikali za kuisogeza elimu ya fedha karibu na wananchi pamoja na kuwajengea wananchi uwezo kuanzia wakiwa wadogo kuelewa matumizi sahihi ya huduma za fedha zinazotolewa kwa ajili ya kujenga uchumi na kuondoa umaskini.

Prof. Mkenda alisema suala la changamoto ya mitaji na namna ya kuunganisha wenye fedha na wanaohitaji mitaji ni muhimu sana, huku akiwaomba wadau wa Sekta ya Fedha nchini kuangali mtaala huo na kutoa maoni yao yatakayoboresha zaidi na kuuwezesha kuleta matokeo tarajiwa.



*Afisa Usimamizi wa Fedha Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Grace Muiyanza, akitoa elimu ya Fedha kwa Machifu na wawakilishi wa vikundi vya kijamii jijini Mbeya, kuhusu utunzaji wa fedha binafsi, umuhimu wa kuweka akiba pamoja na kupanga bajeti na matumizi walipotembelea Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, katika Viwanja vya Ruanda-Nzovwe, Jijini Mbeya.*








# SERIKALI YATILIA MKAZO UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI (PPP) KWA MAENDELEO YA KIUCHUMI

*Na. Josephine Majura*

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikisisitiza kuwa sasa ni wakati wa Sekta Binafsi kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa msisitizo huo kila wakati kuwa pale ambapo Sekta Binafsi inapoweza kutekeleza mradi wa maendeleo, hakuna haja kwa Serikali kutumia fedha zake.

Hivyo, ni wakati sahihi wa Mamlaka za Serikali kutumia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti.

Utaratibu huo utawezesha fedha zilizopangwa kutumika kwenye miradi ambayo inaweza kufanywa na Sekta Binafsi zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo isiyokuwa na mvuto Sekta Binafsi.

Wizara ya Fedha inaunga mkono maono na juhudi za Mheshimiwa Rais kwa kuwaagiza watendaji wa Serikali pamoja na wataalam kuhakikisha miradi yote yenye mvuto wa kutekelezwa na Sekta Binafsi inatekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

Agizo hilo lilitolewa Jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo na Bw. Rashid Ally Salim - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar kwa niaba ya Makatibu Wakuu wa Wizara hizo wakati wa Kikao cha Kuimarisha Ushirikiano katika utekelezaji wa programu ya PPP baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Katika kikao hicho Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha aliwaagiza wataalam hao kukuza uelewa wa dhana ya PPP kwa wadau wake kwa kuwa bado zipo changamoto za uelewa wa dhana hiyo pamoja na faida zake.



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo, akizungumza katika kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu masuala ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Dodoma.*



*Kaimu Kamishna wa Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Wizara ya Fedha, Bw. Bashiru Taratibu, akizungumza katika kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Kazi Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar, Bw. Rashid Ali Salim akizungumza wakati wa kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu masuala ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Dodoma.*

Aidha, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Zanzibar Bw. Rashid Ally Salim na alisisitiza wataalamu kuhakikisha wanayafanyia kazi maazimio yote yaliyoafikiwa katika kikao hicho husus an suala la kuwa na mkakati wa pamoja wa kutangaza fursa na kuibua miradi ya pamoja ya PPP ikiwemo Mradi wa Daraja la Muungano kati ya Dar es Salaam na Zanzibar.

Aidha, Kaimu Kamishna wa Kitengo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Wizara ya Fedha, Bw. Bashiru Taratibu, akizungumza katika kikao hicho alielezea mafanikio yaliyofikiwa na pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa programu ya PPP ambapo kwa Tanzania Bara ina takribani miradi 74 iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na Zanzibar ipo zaidi ya miradi 13 inayotekelezwa.

Vilevile, Kaimu Kamishna alisisitiza umuhimu wa Tanzania kuwa na Sera na Sheria ya PPP itakayowezesha utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Mapendekezo kama hayo kwa nchi za Afrika Mashariki yameanza kufanyiwa kwa kuanza kuandaa Sera ya PPP Afrika Mashariki.




*Meza kuu ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Kazi Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar, Bw. Rashid Ali Salim, wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi kutoka Ofisi ya Rais - Kazi Uchumi na Uwekezaji Zanzibar na Wizara ya Fedha Tanzania Bara baada ya katika kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu masuala Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Dodoma.*

GePG
Government electronic
Payment Gateway




# Tabasamu lako lipo **GePG App**, Fanya Malipo ya Serikali kwa Uhakika na Haraka

Pakua sasa kupitia
App Store na Play Store

# UFANISI WA MPANGO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

*Na. Saidina Msangi*

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni dhana inayowagusa wajasiriamali wadogo yenye lengo la kuwawezesha katika upatikanaji wa mitaji na masoko katika biashara zao.

Kutokana na changamoto za uwepo wa mikopo umiza, riba kubwa kwa wajasiriamali na ucheleweshaji wa mikopo kwa wajarisiamali, Serikali ilikuja na mpango mkakati wa kukabiliana na hilo.

Moja ya mikakati hiyo ni kuanzishwa kwa programu mbalimbali za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ambapo zaidi ya programu 54 zilianzishwa lengo likiwa ni kuwainua wajasiriamali wadogo na wa kati kupata mitaji na masoko.

Miongoni mwa Mifuko iliyoanzishwa ni pamoja na Mfuko wa Halmashauri maarufu kama mikopo ya asilimia 10, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF), Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (AGITF), Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo SELF-MF, pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) na Mingineyo.

Ni ukweli usiopingika kuwa Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanapata mikopo pamoja na usaidizi wa kutumia mikopo hiyo kupitia programu zake za kuwawezeha wajasiriamali wa dogo na wakati kiuchumi.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na Wizara ya Fedha ya kufuatilia ufanisi wa Mifuko na Programu za Serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazolenga wajasiriamali wadogo na wa kati, yanaonesha kuwa sekta isiyo rasmi iliongoza kwa asilimia 68 katika kuwapatia wananchi mitaji.

Matokeo haya yanaonesha kuwa wananchi wapo katika hatari kubwa na kuwa hawana uelewa wa mifuko rasmi ya kuwapatia mitaji jambo linalowaingiza katika mtego wa mikopo umiza yenye riba kubwa ambayo haina manufaa kwao bali kwa watoaji mikopo husika.



Aidha, utafiti huu unaonesha kuwa taasisi za fedha kama vile benki zina mchango mdogo katika kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na hii ni kutokana na wajasiriamali wengi wanashindwa kufikia vigezo vya kupata mitaji na uwepo wa riba kubwa katika urejeshaji wa mitaji hiyo.

Utafiti huo unaonesha kuwa utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali ni asilimia 1.6 pekee ya mitaji inayotokana na taasisi za fedha kama vile benki, pia Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha zinatoa asilimia 1.6, pamoja na programu za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ambazo nazo zinatoa asilimia 1.6 ya mikopo hiyo.

Aidha, Saccoss zinachangia asilimia 3 huku vikundi vya kijamii vikichangia asilimia 10 wakati misaada ikitoa asilimia 13. Matokeo haya yanaashiria kwamba licha ya uwepo wa mifuko rasmi ya utoaji wa mikopo lakini kuna mwamko mdogo katika kupata mitaji kupitia mifuko hiyo.

Licha ya kuwepo kwa takribani programu 54 zilizoanzishwa na Serikali kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ni mifuko miwili pekee ndio inayofahamika zaidi ambayo ni Mfuko wa Halmashauri wa mikopo ya asilimia 10 pamoja na TASAF.

Hata hivyo mifuko hii mingi hupatikana maeneo ya mjini ikichukua asilimia 71 huku upande wa vijijini uelewa wa mifuko hii ni mdogo kwa asilimia 28. Licha ya kuwa na changamoto katika utendaji kazi na ufanisi, mifuko hii imekuwa na matokeo chanya kwa wanufaika kwani imeongeza fursa za ajira.

Kimsingi watu 4,325 sawa na idadi ya watu 11 kwa kila mnufaika walipata ajira kupitia mikopo hii iliyotolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Mafanikio ya programu hizi zinawezesha Serikali kuendelea na mikakati hii ili kupunguza umasikini na kuwawezesha wajasiriamali wodogo.

Hivyo, hatua madhubuti zinatakiwa kuchukuliwa ikiwemo kuongeza utoaji wa elimu na mafunzo ya usimamizi wa biashara, elimu ya usimamizi wa mikopo ili kufanikisha mikopo hiyo ifanye kazi inayotakiwa pamoja na Mifuko iongeze kasi ya kujitangaza zaidi kwa wananchi ili ijulikane kwa urahisi.

Aidha, Mifuko iongeze nguvu kuwafikia vijana ili waweze kujiajiri kwa kupata mikopo hiyo sambamba na utoaji wa elimu ya urejeshaji wa mikopo pamoja na ufuatiliaji wa wanufaika wa mikopo hiyo ili kuwezesha wengine kuingia katika programu hizo.

Aidha, Elimu ya Fedha, inayotolewa na Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zake kupitia Mpango Mkuu wa Maendeleo Sekta ya Fedha 2020/21- 2029/30 unaolenga kufikia wananchi asimia 80 hadi kufikia mwaka 2025/26 pamoja na utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha kwa Umma ya mwaka 2020/21 - 2025/26, ni miongoni mwa nyenzo zitakazowezesha wananchi kufikiwa na elimu ya fedha.

Kupitia utoaji wa elimu hiyo ya fedha iliyoanza mwezi Mei mwaka 2024 ilifikia mikoa 12 na halmashauri 62 ambapo makundi mbalimbali yalifikiwa ikiwamo wajasiriamali, watumishi wa umma na binafsi, wakulima, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu, wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha pamoja na watoa huduma za fedha, walijulishwa juu ya fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali ikiwemo mifuko inayoweza kuwanufaisha kiuchumi.

Tunaamini kuwa Mafanikio ya utekelezaji wa programu ya elimu ya fedha kwa umma yatawezesha wananchi kuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na usimamizi wa fedha binafsi, fursa mbalimbali za mikopo, riba za mikopo, umuhimu wa kuweka akiba ya uzeeni pamoja na kufahamu namna nzuri ya kupanga malengo na vipaumbele kwa kuzingatia kipato cha mwananchi husika.

# UMUHIMU WA SEKTA YA UNUNUZI NA UGAVI KATIKA KUTEKELEZA MIRADI.

*Na. Asia Singano*

Sekta ya ununuzi na ugavi ni muhimu sana katika kuhakikisha Serikali inafanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo jambo linalofanya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi kusisitizwa kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

Katika kuhakikisha kuwa sekta hiyo inatoa mchango uliokusudiwa, Bodi ya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) iliyochini ya Wizara ya Fedha, inaitisha Kongamano la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ambapo mwisho wa mwaka 2024, limefanyika Kongamano la 15 la Wataalam hao, katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano - AICC Jijini Arusha, huku Mgeni rasmi akiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko.



Katika Kongamano hilo Mhe. Doto Biteko, aliwataka Wataalam wa Ununuzi na Ugavi kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia kada ya Ununuzi na Ugavi nchini ili kuhakikisha sekta hiyo inawatoa watu kwenye umasikini.

Mhe. Biteko alisema kuwa Sekta ya Ununuzi na Ugavi ndio eneo pekee linalochukua takribani asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali, hivyo uadilifu pekee ndio utakaosaidia fedha kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa hasa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, Dkt. Biteko aliwaasa Wataalam hao kuzingatia na kuyaishi yale yaliyomo kwenye Sheria za Ununuzi kwa kufanya kazi yenye tija, uwazi na kujiepusha na vitendo vya rushwa kwenye masuala yote ya Ununuzi wa Umma.

> *Serikali iliamua kuanzisha Sheria ya Ununuzi ili kuwa na ununuzi wenye tija, kupata bidhaa zenye ubora, kwa wakati na kuondoa mianya ya rushwa. Hivyo naomba mkutano huu uzingatie yale yanayotafsiriwa kwenye sheria hiyo"alisema Mhe. Dkt. Biteko*

Mhe Biteko aliipongeza Bodi ya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), kwa hatua mbalimbali inazochukua hasa kwa wale wanaoenda kinyume na maadili ya sekta hiyo na kusisitiza kuwa Serikali kupitia Bodi hiyo haitasita kuwachukulia hatua kali watumishi ambao watashindwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria zilizopo.Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko, Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alisema kuwa Wizara ya Fedha imeendelea kuwapa thamani na kutoa kipaumbele kwa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika eneo lao la kazi ili kukuza uchumi.



*Kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 tumewapa hadhi ya kuwa Wakurugenzi, Mameneja n.k kwa kuzingatia ukubwa wa Taasisi Nunuzi na hivi sasa, Wizara inaendelea na jitihada za kurekebisha Muundo wa Vitengo vya Ununuzi na Ugavi ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi" alisema Mhe. Chande.*

Kongamano la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ambalo lilikuwa na kaulimbiu ya Mabadiliko ya Ununuzi na Ugavi kwa Usimamizi Bora wa Rasilimali linafanyika kila mwaka kwa lengo la kutoa fursa kwa Bodi ya Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) kukutana na wataalam wake pamoja na wadau wa mnyororo wa ununuzi na ugavi, ili kujadiliana kwa pamoja jinsi ya kuboresha utendaji kazi katika mnyororo mzima wa ununuzi nchini.

Kwa mwaka 2024 Kongamano la 15 la Watalamu wa Ununuzi na Ugavi lilifanyika kwa siku tatu ambapo kupitia Kongamano hilo mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa Maafisa Ununuzi na Ugavi sambamba na kukumbushwa juu ya wajibu wao na umuhimu wao  huku siku ya tatu Kongamno hilo likifungwa na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha akimwakilisha Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb).

Akizungumza kwa niaba ya Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Bw. Missaile Musa aliwasihi Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kuleta maendeleo ya wananchi kwakuwa ndiyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita Inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Bw. Musa aliongeza kuwa eneo la ununuzi na ugavi ni eneo muhimu katika utendaji wa taasisi nyingine ikiwemo taasisi za Serikali, hivyo wataalam hao wanapaswa kutekeleza wajibu wao na kuondosha vikwazo mbalimbali katika ununuzi na ugavi.

"Niwaombe wataalamu, twendeni katika maeneo yetu ya kazi, tukatimize majukumu yetu kwa weledi zaidi kwa kuondoa changamoto zote zilizojadiliwa hapa ili kuendelea kulisukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu"aliongeza Bw. Musa.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) Bw. Benezeth Ruta, alisema kuwa washiriki walijadili masuala mbalimbali muhimu kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za ununuzi na ugavi ili kuendana na mazingira ya sasa.

*Kongamano la mwaka 2023, lilijielekeza kujadili Mabadiliko ya kidigitali katika kuboresha usimamizi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi kwa maendeleo endelevu" alisema Bw. Ruta.*

Bw. Ruta aliongeza kuwa wataalam hao wa Ugavi na Ununuzi walipata nafasi ya kujadili mada zote zilizowasilishwa na walipata kupanua Mawazo yao juu ya mchango wa fani hiyo katika kukuza uchumi wa viwanda nchini.

**Mwisho**





# MAJIBU YA WIZARA YA FEDHA KUHUSU HOJA ZA WABUNGE, BUNGENI, DODOMA

*Na. Asia Singano*

Katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha ilitoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu majukumu yake ikiwa ni pamoja na Serikali kulipa madeni baada ya uhakiki na upatikanaji wa fedha, kuondoa vikwazo katika ukusanyaji kodi na kuhakiki wastaafu kidijitali.

## NOV 5, 2024 | KUHUSU MSAMAHA WA KODI KWENYE VYAKULA VYA MIFUGO.

Mnamo Novemba 5, 2024, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, alisema kuwa, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imetoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye uingizwaji wa vyakula vya mifugo ikiwemo vyakula vya Samaki vinavyotambulika kwa HS Code 23.09 chini ya utaratibu wa utozaji ushuru wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Dkt. Nchemba alifafanua kuwa, Serikali inaendela kuongea na Sekta ya Mifuko na Uvuvi ili kuona maeneo ambayo yanastahili kupata ruzuku na tayari baadhi ya maeneo Serikali inatoa ruzuku na itaendelea kutoa ruzuku katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Aliongeza kuwa Serikali inaweka vivutio kwenye uzalishaji wa bidhaa ili kujitosheleza ndani ya nchi ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuwa itaangalia maeneo ya maboresho katika bajeti ijayo ili kufanikisha kuongeza uzalishaji wa ndani.

## OCT 29, 2024 | KUONDOA VIKWAZO UKUSANYAJI KODI

Kutokana na umuhimu wa kodi katika kukuza uchumi, Serikali imetatua changamoto mbalimbali za ukusanyaji kodi kwa hiari kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo njia ya kutoa elimu ya kodi kwa wananchi.

Akizungumza Bungeni jijini Dodoma, Oktoba 29, 2024, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alisema Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali dhidi ya mambo yanayokwamisha makusanyo ya kodi, kwa kutoa elimu ya kodi na kuboresha mfumo wa kodi ili kuhakikisha viwango vya kodi vinawiana na hali halisi ya biashara pamoja na kuwahamasisha ulipaji kodi wa hiari.

Mhe. Chande alisema kuwa, Serikali inaendesha kampeni za uelimishaji ili kuwawezesha wafanyabiashara kuelewa umuhimu wa kulipa kodi na mchango wake katika maendeleo ya Taifa ambapo elimu hiyo hutolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina, redio, televisheni, elimu ya mlango kwa mlango, mikutano ya wadau (Stakeholders Forums), pamoja na mitandao ya kijamii.

Aliongeza kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), imekuwa ikijikita kwenye matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha ulipaji kodi unafanyika kwa uwazi na usahihi.



*Matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya kodi yameimarisha uwajibikaji, uwazi, na kuongeza ufanisi wa TRA katika ukusanyaji wa mapato. Hii imepunguza ukwepaji kodi, kuimarisha nidhamu ya walipa kodi, na kurahisisha shughuli za biashara nchini", alibainisha Mhe. Chande.*

Alisema licha ya kuendesha kampeni za uelimishaji na kuimarisha mifumo ya kodi, Serikali ilifanya maboresho ya Sheria za kodi dhidi ya wafanyabiashara na wananchi wanaokwepa kodi ili kuhakikisha wanalipa kodi na kuongeza mapato ya nchi.

*Sheria za kodi zimeimarishwa ili kuhakikisha kuwa hatua kali zinachukuliwa dhidi ya wale wanaokwepa kodi. Adhabu hizi ni pamoja na faini kubwa, kufungwa kwa biashara, au kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa wafanyabiashara watakaobainika kukwepa kodi", alisema Mhe. Chande.*

Vile vile, Mhe. Chande alizishauri taasisi nunuzi nchini kutumia mfumo wa NeST na kuchagua njia ya ununuzi inayoendana na thamani ya mradi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hasa hasa yenye thamani chini ya shilingi millioni 100.

Alitoa ushauri huo wakati akijibu swali la Mbunge wa Malinyi, Mhe. Antipas Zeno Ngusi, aliyetaka kujua kama Serikali inaona umuhimu wa kuondoa miradi chini ya shilingi milioni 100 katika Mfumo wa NeST ili kupunguza ucheleweshaji.

Mhe. Chande alisema kuwa, Mfumo wa NeST umerahisisha masuala ya ununuzi wa umma na unawezesha matumizi ya njia ya ununuzi wa thamani ndogo usiotumia fedha taslimu kwa kazi za ujenzi hadi zenye thamani ya shilingi millioni 100 ambapo kupitia njia hii Taasisi nunuzi inaweza kununua moja kwa moja kutoka kwa muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma bila ya kuhitaji kuwashindanisha wazabuni zaidi ya mmoja.

## NOV 4, 2024 | ULIPAJI MADENI

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Novemba 4, 2024, aliliambia Bunge, jijini Dodoma kuwa Serikali itaendelea na utaratibu wa ulipaji wa madeni mbalimbali ikiwemo madeni ya Wazabuni wa chakula waliotoa huduma katika shule mbalimbali kwa kuzingatia upatikanaji wa mapato baada ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) kufanya uhakiki wa madeni husika.

Hayo aliyasema wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Moshi Mjini Mhe. Priscus Jacob Tarimo (Mb), Mhe. Chande alisema kuwa lengo la Serikali kufanya uhakiki lilikuwa kutekeleza azma ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kulingana na sheria ya Bajeti SURA 439 na Sheria ya Fedha za umma SURA 348.



*Wizara ya Fedha inazielekeza Halmashauri zote nchini kulipia huduma mbalimbali wanazopokea kutoka kwa watoa huduma kwa wakati ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni na kuondoa usumbufu usio wa lazima kwa watoa huduma," alifafanua Mhe. Chande.*

Kwa upande mwingine alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chonga, Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mhe. Chande, alisema kuwa Serikali mbili zinaendelea na mashauriano juu ya mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu utaratibu wa kudumu wa Kuchangia Matumizi na Kugawana Mapato ya Muungano.

Aliongeza kuwa uamuzi wa pamoja utakapofikiwa na pande mbili za Muungano, ndiyo utakaowezesha kufunguliwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja.

## NOV 8, 2024 | UHAKIKI WA WASTAAFU KIDIJITALI.

Katika kuwarahisishia wastaafu wanaolipwa na Hazina, Serikali inatengeneza mfumo wa kidigitali utakaowawezesha Wastaafu kujihakiki wenyewe (Self verification) kupitia simu zao za mkononi au kwa kutumia huduma za kibenki ili kuwapunguzia Wastaafu gharama na usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kwenda kuhakikiwa.

Hayo yalielezwa bungeni jijini Dodoma, Novemba 8, 2024. Na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nachingwea, Mhe. Amandus Julius Chinguile, aliyehoji sababu za Serikali isiweke utaratibu wa Wastaafu kuhakikiwa kwenye Halmashauri au Kata badala ya utaratibu wa sasa wa kuhakikiwa Mikoani.

Mhe. Chande alisema uhakiki wa wastaafu wanaolipwa na Hazina umekuwa ukifanyika katika ngazi ya Halmashauri, hata hivyo, ili kuwapunguzia Wastaafu gharama na usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kwenda kuhakikiwa, Serikali inatengeneza mfumo wa kidigitali utakaowawezesha Wastaafu kujihakiki wenyewe.

Alisema baada ya kukamilika kwa taratibu zote, Wastaafu watapewa elimu ya jinsi ya kujihakiki wenyewe na watatangaziwa siku ya kuanza kujihakiki.

Alitoa maelezo hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Wingwi, Mhe. Omar Issa Kombo, aliyetaka kujua wakati ambao Serikali itajenga Benki za NMB na CRDB kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Chande alisema kuwa uamuzi wa kufungua matawi ya benki hufanywa na benki yenyewe ambapo kabla ya kufanya uamuzi huo, benki hufanya upembuzi yakinifu ukiwa na lengo la kuangalia kama kuna uwepo wa biashara ya kutosha ambayo italeta faida.

Aliongeza kuwa Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT), haina kizuizi chochote katika suala la mabenki kufungua matawi, kama benki husika itatimiza masharti yote ya kufungua matawi kama yalivyoainishwa katika Kanuni Namba 31 ya Kanuni za Utoaji Leseni za Mabenki na Taasisi za Fedha za Mwaka 2014.

Mhe. Chande alibainisha kuwa Benki za NMB na CRDB hazina matawi kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Micheweni lakini, wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanapata huduma za kibenki kutoka benki za CRDB na NMB kupitia mawakala wa benki, ambapo hadi kufikia Oktoba 2024, kulikuwa na jumla ya mawakala 4 wa Benki ya CRDB na 14 wa Benki ya NMB wanaotoa huduma za kibenki katika Wilaya hiyo.

*Benki zikishafanya upembuzi yakinifu katika sehemu husika huwasilisha uamuzi/pendekezo lao Benki Kuu ya Tanzania", alisema Mhe. Chande.*





# SERIKALI NA IMF ZINAVYOKABILI MABADILIKO YA TABIANCHI

*Na. Peter Haule*

Tanzania kama nchi nyingine duniani imekuwa ikikabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa miongo kadhaa ambayo yanahusishwa kwa karibu na ongezeko la joto duniani, shughuli za binadamu kama vile ukataji miti, uzalishaji wa gesi chafuzi, na matumizi yasiyofaa ya ardhi.

Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa kuanzia miaka ya 1960, wastani wa joto nchini umeongezeka kwa takribani nyuzi joto moja jambo ambalo limeathiri majira ya mvua, uzalishaji wa mazao, kuongezeka kwa ukame, kupanda kwa kiwango cha maji ya bahari na kupungua kwa barafu ya Mlima Kilimanjaro tangu miaka ya 1900.

Changamoto hizi zinahitaji juhudi za mtu mmoja mmoja, Serikali na wadau wa maendeleo hususani mashirika ya kimataifa na Benki ikiwemo Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika kuzitatua.

Shirika la Fedha la Kimataifa iliitangaza Tanzania kuwa nchi ya pili, baada ya Madagasca kunufaika na Mfumo wa Ushirikiano wa Kuimarisha Hali ya Hewa kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari mbaya za uharibifu wa mazingira.

Kunufaika kwa Tanzania kupitia mashirika ya kimataifa hususani IMF kunatokana na juhudi za kimkakati zinazofanywa na Serikali kupitia Sera zake za ndani na nje zinazoimarisha ushirikiano wa kimaendeleo katika sekta mbalimbali zikiwemo za kiuchumi na kijamii.

Kupitia Mfumo wa Ushirikiano wa Kuimarisha Hali ya Hewa kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na

athari mbaya za uharibifu wa mazingira, IMF na World Bank Group (WBG) wanafanya kazi kwa karibu na washirika wengine wa maendeleo, kuratibu juhudi zao za kuunga mkono ajenda ya mageuzi ya sera ya Tanzania ili kukabiliana na vihatarishi na changamoto zinazohusiana na mabadiliko hayo ya tabianchi na kuimarisha ustahimilivu wa uchumi wa Tanzania.

Kiongozi wa Timu ya Wataalam kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa, Bw. Charalambos Tsangarides, alisema kuwa kupitia mpango huo, IMF itaunga mkono kuanzishwa kwa kanuni za uwekezaji wa umma zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na utoaji taarifa, huku Benki ya Dunia ikijikita katika kusaidia kutekeleza miradi katika sekta zitakazoimarisha uwezo wa Tanzania kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama vile nishati, maji, hifadhi ya jamii na kilimo.



*Kiongozi wa Msafara wa Timu ya Wataalam kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Bw. Charalambos Tsangarides, akizungumza katika kikao kilichawakutanisha Timu yake na Wizara ya Fedha, Jijini Dodoma.*

Katika kusisitiza ushirikiano huo wenye manufaa kwa Tanzania, Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bw. Nathan Belete, akizungumza kwa njia ya mtandao kutoka Washington D.C, nchini Marekani, alisema kuwa Tanzania itanufaika na msaada wa kiufundi na kifedha kutoka taasisi hizo mbili katika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu itakayokuza uzalishaji, kuhifadhi mazingira na kuwa na mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) pia limekuwa likichangia maendeleo ya Taifa kupitia misaada na mikopo nafuu inayoipatia Tanzania kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kukuza uchumi wa nchi.

Akifungua vikao vya majadiliano kati ya Serikali na Timu ya Wataalam kutoka (IMF) iliyowasili nchini kufanya Tathimini ya Awamu ya Nne ya utekelezaji wa Program ya Extended Credit Facility-(ECF), inayohusisha upatikanaji wa mkopo nafuu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na huduma Mwezi Oktoba 2024, Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alisema kuwa Tanzania inatekeleza Program ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia Programu ya Resilient and Sustainable Fund (RSF) baada ya kukidhi vigezo



*Baada ya kutekeleza kwa mafanikio programu nyingine zilizopita ikiwepo ile ya Dirisha la Dharura ambapo tulipata fedha za kukabiliana na athari za UVIKO-19 (Rapid Credit Facility- (RCF)), na huu wa ECF unaolenga kufufua na kuimarisha uchumi, Tanzania imetimiza sifa ya kutekeleza programu ya RSF ambapo tutapata fedha za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutoka IMF," alisema Dkt. Nchemba.*

Vilevile ushirikiano huo na Mashirika ya Kimataifa unatakiwa kuimarishwa pia na Benki Kuu za nchi za Afrika kwa kuweka mipango na mikakati ya kutafuta fedha kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo sekta binafsi kwa ajili ya kukabiliana na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi katika nchi hizo.

Akizungumza katika mjadala uliofanyika kando ya Mikutano ya Mwaka ya WB na IMF, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba alisema kuwa Benki Kuu za

nchi za Afrika zinawajibu wa kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alizitaja mbinu mahususi ikiwemo uanzishwaji wa hati fungani za kijani zenye lengo la kuvutia uwekezaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na kusimamia ipasavyo Taasisi za fedha kuwekeza kwenye kilimo kwa kutoa mikopo, itakayosaidia kukuza uchumi wa nchi hizo za Afrika na maendeleo ya watu wake.

Alibainisha kwamba mabadiliko ya tabianchi yameziathiri nchi nyingi ikiwemo Tanzania na kwamba upatikanaji wa fedha kwa njia shirikishi katika kukabiliana na athari hizo kutaimarisha uchumi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Macroeconomic and Financial Management of Eastern and Southern Africa (MEFMI), Dkt. Louis Kasekende, alisema kuwa Taasisi yake imejipanga kuwawezesha wanachama wake kuweka mipango ya pamoja ya kutafuta fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa uhimilivu wa madeni ya nchi za Afrika.

Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari kubwa kwa Tanzania, hasa katika sekta za kilimo, maji, na mazingira. Juhudi zinazochukuliwa na Serikali na wadau mbalimbali kwa kuweka mikakati ya kupunguza athari hizi kwa kutumia mbinu endelevu kama kilimo bora, uhifadhi wa mazingira, matumizi ya nishati mbadala, na uhamasishaji wa jamii zinaleta matumaini mapya kwa kizazi cha sasa na kijacho.




*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (mwenye nguo nyekundu), akiwa katika mjadala uliofanyika kando ya Mikutano ya Mwaka ya WB na IMF, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, kuhusu Mabadiliko ya Tabia nchi.*



# USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KULETA TIJA KATIKA BIASHARA NA UWEKEZAJI TANZANIA

*Na. Saidina Msangi*

Wahenga wanasema! Ukitaka kufika haraka tembea mwenyewe na ukitaka kufika mbali tembea na wengine. Kauli hii inajidhihirisha katika juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhakikisha kuwa inashirikiana na mataifa mengine ili kupiga hatua za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kauli hiyo inadhihirishwa zaidi na ziara ya Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (MB), aliyeongoza ujumbe wa Tanzania katika ziara ya kikazi katika nchi za Saudi Arabia na Serikali ya Kisultan ya Oman.

Pamoja na mambo mengine, malengo makuu ya ziara hiyo yalikuwa ni kusaini Mkataba wa Kuondoa Utozaji Kodi ya Mapato Mara Mbili na Kuzuia Ukwepaji Kodi (Agreement for the Elimination of Double Taxation with Respect to Taxes on Income and Prevention of Tax Avoidance and Evasion- DTA), kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Oman pamoja na kushiriki Kongamano la Biashara na Uwekezaji, lililofanyika Mjini Riyadh, nchini Saudi Arabia.

Serikali ya Tanzania na Serikali ya Kisultan ya Oman zilisaini Mkataba wa Kuondoa Utozaji Kodi ya Mapato Mara Mbili na Kuzuia Ukwepaji Kodi tarehe 15 Desemba, 2024, nchini Oman. Mkataba huo ulisainiwa na Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), kwa niaba ya Serikali Tanzania na Bw. Nasser Khamis Al - Jashmi - Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mapato ya Oman, kwa niaba ya Serikali ya Oman.

Kusainiwa kwa mkataba huo ni hatua muhimu katika jitihada za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kufungua uchumi wa nchi kwa kuvutia uwekezaji wa kimataifa kwa kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara wanaofanya shughuli kati ya Tanzania na Oman kutozwa kodi mara moja pekee, badala ya kutozwa mara mbili kwa mapato ya aina moja.



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akisaini Mkataba wa Kuondoa Utozaji Kodi ya Mapato Mara Mbili na Kuzuia Ukwepaji Kodi,  Kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Kisultan ya Oman, iliyowakilishwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mapato ya Oman, Bw. Nasser Al-Jashmi.*

Mkataba huu pia unalenga kuvutia mitaji mikubwa kutoka Oman kuja kuwekezwa nchini Tanzania, hususan kupitia kampuni kubwa zinazomilikiwa na familia za kifalme, sambamba na wawekezaji binafsi. Kupitia uwekezaji huo, Tanzania inatarajia kunufaika na ukuaji wa sekta za uzalishaji, maendeleo ya viwanda, na kuongezeka kwa ajira kwa wananchi.

Vile vile, kusainiwa kwa mkataba huo, kunatarajiwa kufungua ukurasa mpya wa ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Oman, huku Oman ikivutiwa zaidi na fursa za uwekezaji nchini Tanzania kutokana na jiografia yake ya kimkakati, vivutio vyake vya kiuchumi, na mazingira bora ya uwekezaji ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Tanzania pia inaendelea na ushirikiano na nchi ya Saudi Arabia, uliodumu kwa takribani miaka 40, ukiinufaisha Tanzania ambapo imeweza kupata ufadhili kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saudi Fund for Development-SFD), katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta za maji, afya, nishati na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), alipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Saudi Fund, Bw. Sultan Al-Mashard, Kando ya Mkutano wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji, lililofanyika Mjini Riyadh nchini Saudi Arabia, lililokuwa na lengo la kupanua wigo wa biashara na uwekezaji kati ya nchi ya Tanzania na Saudi Arabia.

Dkt. Nchemba aliitaja baadhi ya miradi iliyoleta mageuzi makubwa katika jamii ya Tanzania kuwa ni  pamoja na ukarabati wa Mradi wa Maji mkoani Mara (Usd 15m), Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe (Usd 25m), na ujenzi wa Barabara za Vijijini Awamu ya Pili-Zanzibar (Usd11.4m), ukarabati na upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja-Zanzibar (Usd 15m) na kushirikiana na wadau wengine kufadhili Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Umeme wa msongo wa 220kV kuanzia Benako hadi Kyaka (Usd 105.4m).



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saudi Fund for Development-SFD), Bw. Sultan Al-Marshad, Mjini Riyadh nchini Saudi Arabia.*

Katika Mazungumzo hayo, Dkt. Nchemba aligusia utekelezaji wa miradi mingine mikubwa ya kimkakati inayoendelea nchini Tanzania ukiwemo mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), ambao alisema utakapokamilika utakuwa kichocheo kikubwa cha biashara na Uchumi katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Saudi Fund, Bw. Sultan Al-Marshad, alisema kuwa Mfuko huo uko tayari kuendelea kuisaidia Tanzania kutokana na uhusiano imara uliopo kwa faida ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Alipongeza hatua kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kutekeleza miradi muhimu kwa maendeleo ya nchi akiitaja reli ya kisasa inayojengwa kwamba itachochea na kukuza biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo katika eneo la mradi.

Pia Dkt. Nchemba alipata fursa ya kufanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Wizara ya Uchumi na Mipango wa Saudi Arabia, Eng. Ammar Naqadi, Kando ya Mkutano huo wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji, lililoandaliwa na Ubalozi wa Tanzania, kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Shirika la Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Dkt. Nchemba alitumia fursa hiyo kuikaribisha Saudi Arabia kuwekeza Tanzania katika fursa mbalimbali zikiwemo utalii, madini, uendelezaji wa miundombinu, uchumi wa buluu na kilimo ambapo ina ardhi ya kutosha na yenye rutuba kuweza kuzalisha mazao ya aina mbalimbali kwa wingi.

Alibainisha kuwa Tanzania inaendelea na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambapo imeshakamilika kwa



asilimia mia moja, kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na ujenzi unaendelea kwa vipande vinavyoelekea Mwanza na DRC kupitia Burundi, hivyo ni fursa kwa Saudi Arabia kuwekeza katika miundombinu hiyo ambayo itachochea ukuaji wa bishara kati ya Saudi Arabia, Tanzania na nchi za Afrika Mashariki.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, alisema kuwa Zanzibar ina fursa zinazoweza kutumiwa na Saudi Arabia ikiwemo sekta ya utalii wa fukwe za asili zilizopo Zanzibar, fursa ya uvuvi wa kina kirefu na uchakataji wa mazao ya uvuvi pamoja na uwepo wa vyanzo vya gesi na mafuta vilivyogunduliwa ni fursa muhimu kwa Saudi Arabia kutokana na uzoefu wake katika sekta hiyo.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Uchumi na Mipango wa Saudi Arabia, Eng. Ammar Naqadi alisema kuwa Saudi Arabia iko tayari kushirikiana na Tanzania katika uendelezaji wa miundombinu ya reli ili kurahisha usafirishaji wa watu, mazao na mizigo ili kuchochochea ukuaji wa biashara ambapo ushiriki wa sekta binafsi ni muhimu katika kufanikisha biashara kati ya nchi hizo mbili.

Alisema nchi hiyo iko tayari kushirikiana na Tanzania katika fursa za kuendeleza sekta ya madini, kilimo, mafuta na gesi, utalii, uchakataji wa mazao ya bahari, miundombinu pamoja na utalii ambapo wataandaa Timu ya wataalamu kwa kushirikiana na Sekta binafsi kutembelea Tanzania kujionea fursa za uwekezaji katika sekta hizo ili kujiridhisha na mazingira ya fursa za Tanzania ili kuweza kuwekeza.




# MKUTANO WA WAHASIBU WAKUU AFRIKA MATOKEO YA SERA BORA ZA SERIKALI

*Na. Peter Haule*

Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mkuu wa Pili wa Wahasibu wa Serikali Barani Afrika, uliofanyika Desemba, 2024 jijini Arusha, ukiwakutanisha zaidi ya wajumbe 2,000 kutoka nchi zaidi ya 55 za Bara la Afrika, ulioangazia pamoja na mambo mengine, kujifunza namna Tanzania ilivyopiga hatua kubwa katika matumizi ya mifumo ya fedha.

Mkutano huo ambao pia ulizikutanisha Jumuiya za wafanyabiashara, ulitoa fursa ya kujua ni namna gani Afrika ipo tayari katika suala la uwekezaji na namna ya kuripoti hali ya uchumi ya Afrika.

Hii inathibitishwa kupitia shuhuda mabimbali za ndani na nje ya nchi ambazo zimelenga Sera bora za kiuchumi na kijamii zilizoifanya Tanzania kuwa kivutio kwa wageni ambao wanatamani kufanya mikutano na pia kujifunza mifumo mbalimbali ya fedha na usimamizi wake.

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, akizungumza katika Mkutano huo, alisema kuwa viongozi, hususani wa Serikali ya Tanzania wamekuwa wakiimarisha mifumo ya kitaasisi na usimamizi wa fedha za umma, kuhakikisha uwajibikaji katika kila ngazi, na kuendeleza dhana ya uwazi barani Afrika.

*Tanzania ipo vizuri katika kutekeleza viwango vya kimataifa vya kihasibu, imekuwa ya mfano katika ukuaji wa Uchumi, imeimarika katika suala la ukarimu wa wageni, maendeleo katika teknolojia ya Habari na Mawasiliano na ni miongoni mwa nchi zenye vivutio vingi vya utalii", alisema Mwenyekiti wa Umoja wa Wahasibu wa Afrika, ambaye pia ni Mhasibu Mkuu wa nchi ya Lesotho, Bi. Malehlohonolo Mahase*





*Kupitia sera nzuri zinazotekelezwa nchini tunapata msukumo wa kufuata viwango vya juu vya huduma, uadilifu, na ubunifu, sifa ambazo zinaendana na maono ya Umoja wa Wahasibu Wakuu wa Serikali wa Afrika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na nyie Wasaidizi wake kwa kutuheshimisha kupitia maono yenu yanayotutia moyo na kuhamasisha juhudi zetu", alisema Dkt. Nchemba.*




Alisema kuwa wajumbe waliohudhuria mkutano wa Pili wa Wahasibu Wakuu Afrika wanawakilisha hazina ya uzoefu, uaminifu, na maono ya kimkakati yanayohitajika kukabiliana na changamoto ngumu za kifedha zinazozikabili nchi za Afrika.

Ushiriki wa dhati wa wahasibu katika mkutano huo ulikuwa na umuhimu katika kuimarisha usimamizi bora wa fedha barani Afrika na pia kutoa mwanga wa matumaini kwa juhudi za pamoja za kujenga msingi imara kwa maendeleo endelevu ya bara la Afrika.

Mkutano wa Wahasibu Wakuu Afrika ulikuwa na kaulimbiu ya "Kujenga Imani ya Umma katika Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa Ukuaji Endelevu", imekuwa nguzo muhimu katika kukuza uwazi, uwajibikaji, na umakini katika matumizi ya fedha ikiwa ni pamoja na kuakisi matarajio ya pamoja kama mataifa ya Afrika ya kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha kama chachu ya ukuaji endelevu.

Kutokana na sifa lukuki ya Tanzania katika jamii za kimataifa, iliweka rekodi ya washiriki zaidi ya 2,000, idadi ambayo inatajwa kuwa ni kubwa kuwahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika -AAAG ambapo mkutano uliotangulia uliofanyika Lesotho ulikuwa na washiriki 1,200.

Aliyekuwa mwenyeji wa Mkutano ambaye ni Mhasibu Mkuu wa Serikali, CPA. Leonard Mkude, alisema kuwa mkutano ulileta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii pamoja na kuitangaza sekta ya utalii ya Tanzania kupitia kwa wajumbe waliotembelea vivutio vya utalii vilivyoko katika ukanda wa Kaskazini ikiwa ni pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Ngorongoro, Mlima Kilimanjaro lakini pia vivutio vilivyopo Zanzibar.

Mkutano ulisaidia viongozi na watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na viongozi na watumishi kutoka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kuleta maarifa mapya katika masuala ya uhasibu kwa njia ya kidigitali.

*Mkutano uliwaleta pamoja na kuwa na maono ya mwamko wa Afrika na Afrika yenye utawala bora, demokrasia, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria, Afrika yenye amani na usalama na Afrika yenye utambulisho thabiti wa kitamaduni, urithi wa pamoja na maadili", alisema CPA. Mkude*



Kupitia mkutano huo, washiriki walipata fursa ya kupata ufahamu kutoka kwa wataalam wa sekta ya umma kuhusu mwelekeo wa kisasa, changamoto, na ubunifu katika usimamizi wa fedha za umma.

Alisema mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya kidijitali katika ufanisi wa sekta ya umma hadi kupambana na mtiririko haramu wa fedha na kutumika moja kwa moja katika majukumu ya kila siku ya wahasibu na wataalamu wa fedha.

Akizungumza wakati wa kufunga Mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, aliwaasa wahasibu kusimamia taaluma yao kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma, na kujiongezea ujuzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Naye Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), akizungumza katika mkutano huo aliwataka wahasibu wote barani Afrika, kuwa waaminifu na kuzisaidia nchi zao katika kuhakikisha zinapata maendeleo.

Alisema kuwa kazi zozote zinazofanywa hususan za miradi ya maendeleo katika nchi za Bara la Afrika zinawahusisha wahasibu hivyo, wazingatie maadili ya taaluma zao na miongozo inayotolewa katika nchi zao ili kuhakikisha malengo yanayopangwa yanafanikiwa.








*"Nataka niwaombe wahasibu mtambue kuwa taaluma yenu ni muhimu hata chochote kinachotokea katika sehemu zenu za kazi mtalaumiwa, hivyo mzuie hasara zinazoweza kutokea" amesema Dkt. Biteko.*

Baada ya kumalizika kwa Mkutano Mkuu wa Pili wa Wahasibu wakuu wa Serikali Afrika, (African Association of Accountants General (AAAG)) nchini Tanzania, Mkutano wa Tatu wa Jumuiya hiyo kwa mwaka 2025 unatarajiwa kufanyika nchini Ghana.



# SERIKALI YABORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA KODI NCHINI

*Na. Eva Ngowi*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ilifanya Makongamano ya Kodi Kikanda, yaliyofunguliwa rasmi tarehe 18 Novemba 2024, ambayo ni Kanda ya Kati (Dodoma) na kuendelea katika Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza na Kigoma), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya na Iringa), Kanda ya Kusini (Mtwara) na kumalizika katika Kanda ya Pwani jijini Dar es Salaam.

Makongamano haya ni sehemu ya juhudi za kudumu za Serikali za kuboresha mfumo wa kodi, kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali kutoka Sekta za Umma na Binafsi ili kutoa maoni kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi nchini.

Katika ufunguzi wa Kongamano la kwanza lililofanyika Kanda ya Kati, jijini Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uchambuzi wa Sera, Bw. William Mhoja, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta binafsi, wataalamu wa kodi, na wadau mbalimbali ili kuboresha mfumo wa kodi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema kuwa ni muhimu kwa Serikali kuendelea kufanya marekebisho katika Sheria na Kanuni zinazohusu kodi ili kuweka mazingira bora ya biashara na kuvutia uwekezaji.

Aidha, alisisitiza kuwa Serikali inaendelea kutekeleza mikakati madhubuti ya kuboresha mazingira ya biashara, jambo ambalo ni muhimu katika kuvutia mitaji ya ndani na nje ya nchi, hali inayochochea ukuaji wa uchumi.

Alitoa mfano wa baadhi ya marekebisho yaliyofanyika katika sekta ya kodi, kama vile kuboresha kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kupunguza ushuru wa bidhaa, na kutoa msamaha wa kodi kwa zana na vifaa vya kilimo, hatua ambazo zinachangia katika kukuza sekta mbalimbali za uchumi.



Makongamano haya pia yalijikita katika kujadili changamoto zinazozikumba sekta za kiuchumi nchini, na namna bora ya kushughulikia changamoto hizi kupitia mfumo wa kodi.

Katika hotuba yake, Bw. Mhoja alieleza kuwa Serikali imejizatiti kupambana na changamoto za kimataifa, kama vile mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinakusanywa na kutumika kwa ufanisi katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Alisisitiza pia kuwa juhudi za Serikali za kuboresha usimamizi wa kodi ni sehemu muhimu ya mikakati yake ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya kijamii, kama vile huduma za afya, elimu, na miundombinu. Hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za kijamii, huku ikizingatia maslahi ya wananchi wa kawaida na wafanyabiashara wadogo.

Katika ukusanyaji wa maoni katika Kanda tofauti tofauti, ilibainika namna ambavyo sekta binafsi inavyotambuliwa kama mhimili muhimu katika kukuza uchumi wa nchi.

Serikali inaendelea kuweka mikakati inayolenga kuboresha mazingira ya biashara ili sekta hiyo iweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kitaifa. Hii ni pamoja na kufuta ada na tozo kero 379, hatua ambayo imetia moyo sekta binafsi na kuongeza ushirikiano kati ya Serikali na wawekezaji.

Makongamano ya Kodi Kikanda pia yalijadili mikakati ya kuongeza




*Kamishna Msaidizi Idara ya Sera Wizara ya Fedha na Mwenyekiti wa Kongamano la Kodi, Bw. Juma Mkabakuli, akifungua Kongamano la Kodi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoani Mbeya kwa niaba ya Uongozi wa Wizara.*

ufanisi katika mfumo wa kodi, na kuzitaja baadhi ya hatua zilizochukuliwa, kama vile kutunga Sheria na Kanuni mpya zinazohusiana na masuala ya msamaha wa kodi kwa vifaa vya kilimo, na kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa muhimu za kimsingi, kama vile maji ya kunywa.

Hatua hizi ni ishara ya dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa sekta binafsi inaendelea kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi, huku ikizingatia mazingira bora kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Miongoni mwa changamoto zinazozikumba juhudi hizi ni mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula, masuala ambayo hayakusahaulika katika mijadala ya Makongamano hayo.

Hizi ni changamoto za kimataifa zinazohitaji juhudi za pamoja kati ya Serikali, sekta binafsi, na wananchi. Serikali ya Tanzania imejizatiti kuhakikisha kuwa inakusanya mapato ya kutosha kutoka kwenye rasilimali zake za ndani na kuzitumia katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Hii ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kutumia teknolojia ya kisasa, ili kupunguza utegemezi wa fedha za kigeni, na kuhakikisha kuwa rasilimali za taifa zinawanufaisha wananchi wote.

Kwa ujumla, Makongamano hayo ya Kodi Kikanda yamekuwa ni jukwaa muhimu la kujenga ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, na wadau wengine, na kuhamasisha juhudi za pamoja katika kukuza uchumi wa taifa.



*Wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara, wajasiriamali wadogo, sekta ya kilimo, biashara za usindikaji wa mazao na washauri wa kodi wakisikiliza wasilisho (halionekani pichani) lililotolewa na Mchumi Mkuu kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Mathias Kadebe,(aliyesimama) kuhusiana na maoni yaliyofanyiwa kazi katika Makongamano ya Kodi yaliyopita yaliyofanyika kikanda.*

Kama inavyofahamika, kodi ni msingi wa maendeleo na kupitia mfumo wa kodi unaohusisha ushirikiano wa pande zote, Tanzania inatarajiwa kufikia malengo yake ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mikakati iliyozungumziwa, kama vile marekebisho katika sekta ya kodi, ni hatua muhimu zinazoweza kuleta matokeo chanya katika kukuza uchumi, huku Serikali ikiendelea kutoa msukumo katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kuanzishwa kwa Makongamano haya ya Kodi Kikanda kumeleta tija katika maboresho ya mfumo wa kodi ambapo katika maandalizi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25 ushirikishwaji wa wadau uliongezeka zaidi.

Ni matumaini ya Serikali ya Tanzania kuwa, Makongamano haya yataendelea kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana mawazo na kujenga mikakati bora ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kwamba kwa ushirikiano wa pamoja, malengo ya maendeleo ya Taifa yatakamilika kwa ufanisi.



*Mjasiriamali wa Viwanda Vidogo vya Kusindika Unga wa Mayai, Bi. Elizabeth Kalinga, akitoa maoni kuhusiana na maboresho ya kodi kwenye viwanda vidogo vidogo, wakati wa Kongamano la Kodi, lililofanyika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoa wa Mbeya.*



*Mfanyabiashara kutoka Kampuni ya Bonafides Voyage Ltd, Bi. Ranjan Suchak, akitoa maoni yake kuhusiana na maboresho ya kodi katika Bajeti ijayo 2025/2026, wakati wa Kongamano la Kodi lililofanyika Kanda ya Pwani, jijini Dar es Salaam.*

# SERIKALI NA HATUA ZA KUKABILIANA NA MIKOPO UMIZA

*Na. Chedaiwe Msuya.*

Katika jamii nyingi zinazoendelea barani Afrika, mikopo imekuwa nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kukuza biashara ndogo na za kati sambamba na maendeleo ya kilimo hususani katika maeneo ya vijijini.

Mikopo hiyo imegeuka shubiri kwa baadhi ya watu kutokana na kukiukwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo na kusababisha mikopo kuwa kero kwa wakopaji na kubatizwa jina la mikopo umiza au kausha damu licha ya uwepo wa taasisi rasmi zinazotoa mikopo kwa masharti nafuu.

Mikopo umiza ni mikopo inayotolewa kwa riba kubwa na masharti kandamizi yanayomuumiza mkopaji badala ya kumsaidia ambapo watu wengi, hasa wale wenye kipato cha chini, wameathirika na aina hii ya mikopo kutokana na ukosefu wa elimu ya kifedha, hali ngumu ya maisha, na ugumu wa kupata mikopo kutoka taasisi rasmi kama benki.

Makala hii imechambua maana ya mikopo umiza, chanzo chake, sababu zinazowafanya wananchi kuingia kwenye mikopo hii, athari zake kwa jamii, na suluhisho la kudumu ili wananchi waachane na mikopo hiyo isiyokuwa ya msingi.

Kama nilivyoainisha huko juu, mikopo umiza ni aina ya mikopo inayotolewa kwa riba kubwa, masharti kandamizi, na muda mfupi wa marejesho ambayo hutolewa na taasisi zisizo rasmi, watu binafsi, au hata baadhi ya kampuni za kifedha zisizo fuata sheria za kifedha zilizowekwa na mamlaka husika.



*Kuchukua mikopo bila kujua unachoingiza, ugumu wa kupata mikopo rasmi kupitia Benki na taasisi za fedha rasmi kutokana na masharti magumu kama dhamana, historia ya kifedha na vigezo vingine ambavyo watu wa kipato cha chini hawawezi kutimiza, ndiyo kichocheo cha watu kukimbilia mikopo ya haraka inayopatikana kwa riba kubwa na masharti kandamizi", alisema Dionesia Mjema, Kamishna Msaidizi wa Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, kutoka Wizara ya Fedha.*



Mikopo umiza mara nyingi hufanya maisha ya mkopaji kuwa magumu zaidi kwa sababu ya mzigo wa riba inayokua kwa kasi na kushindwa kulipa kwa wakati, hali ambayo husababisha unyanyasaji wa kifedha, kupoteza mali na hata kufilisiwa.

Kuna sababu nyingi zinazochangia kuwepo kwa mikopo umiza, ambazo ni pamoja na wananchi wengi kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu masuala ya kifedha, hususan kuhusu mikopo, riba, na athari zake.

Aidha hali ngumu ya kiuchumi, kupanda kwa gharama za maisha na kipato kidogo, huwalazimisha watu kukopa ili kukidhi mahitaji ya msingi kama chakula, ada za shule, matibabu, tamaa ya pesa za haraka.

Watu wengine hukopa kwa matarajio ya kupata faida ya haraka, hasa wafanyabiashara wadogo lakini wanaposhindwa kurejesha hujikuta katika matatizo makubwa ya kifedha lakini pia changamoto ya udhibiti wa taasisi ambapo baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo hutumia njia ya mitandao ya kidigiti, hivyo kusababisha kufanya kazi kiholela na kuwanyonya wananchi.

Madhara ya mikopo umiza ni pamoja na umasikini wa kudumu, kupoteza mali na biashara, msongo wa mawazo na afya mbaya, kudhalilika kijamii na kutumbukia katika uhalifu.

Mfano halisi wa athari za mikopo umiza ni kwa Mama Asha ambaye ni mfanyabiashara mdogo wa kuuza mboga sokoni ambaye alikopa Tsh 500,000 kutoka kwa wakopeshaji wa mtaani kwa masharti kwamba atalipa Tsh 800,000 ndani ya miezi miwili baada ya kushindwa kulipa kwa wakati wakopeshaji walichukua jokofu na bidhaa zake zote alizoweka kama dhamana.

Ili kutokomeza tatizo la mikopo umiza, hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni pamoja na kuimarisha elimu ya kifedha ambayo hivi sasa inafanywa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Taasisi zake, kupanua fursa za mikopo rasmi, kujiunga na vikundi vya kifedha vilivyosajiliwa, kuweka akiba na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na Serikali kuendelea kudhibiti wakopeshaji haramu.










## Tufuate sasa kwenye **Kurasa zetu za Mitandao ya kijamii**

- Facebook: @mofURT
  Wizara ya Fedha
- LinkedIn: Ministry of
  Finance-Tanzania
- X: @mofURT
  Ministry of Finance
  Tanzania
- WhatsApp: Wizara ya Fedha
  Tanzania
- Instagram: @mofURT
  Wizara ya Fedha
- YouTube: @mofURT
  Hazina TV - Wizara
  ya Fedha

**au kupitia Tovuti yetu** | www.mof.go.tz

# MATUKIO **YALIYOJIRI**



MATUKIO YALIYOJIRI

MATUKIO YALIYOJIRI

> *Takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwezi Agosti mwaka 2024, zinaonesha kuwa uchumi wetu umeimarika licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali huku ukuaji huo ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za ujenzi, kilimo, fedha na sekta ya bima" Mhe. Dkt. Nchemba.*








# USHIRIKIANO WA TANZANIA NA OMAN KATIKA MAENEO MUHIMU YA MAENDELEO




*Na. Joseph Mahumi*

Tanzania na Oman zimekubaliana kuendeleza ushirikiano katika Nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo, katika Sekta ya Nishati na Madini, kutengeneza mazingira bora ya uwekezaji baina ya nchi hizo, Ushirikiano wa mafunzo katika masuala ya Kodi pamoja na kuondoa Utozaji kodi mara mbili kwa wawekezaji na wafanyabiashara watakaofanya shughuli zao kati ya nchi hizo mbili.

Makubaliano hayo yamefanyika wakati Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Oman nchini Tanzania, Mhe. Saud Al-Shidhani, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Mhe. Dkt. Nchemba, alisema kuwa ajenda kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha inawezesha sekta binafsi kuwa na nguvu, sambamba na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, hivyo ushirikiano baina ya nchi hizo utaendelea kunufaisha sekta binafsi na wawekezaji kwa kiasi kikubwa.

*Serikali zetu mbili zimeanzisha Tume ya Kudumu ya Pamoja ambayo chini yake tunataja maeneo ya ushirikiano kati ya nchi zetu mbili, ikiwemo biashara na uwekezaji, hivyo natarajia kuwa na fursa ya kupanua zaidi ushirikiano wetu wa maendeleo kwa manufaa ya watu wetu" alisema Dkt. Nchemba*

Aliongeza kuwa, kuna haja ya kubadilisha uwezo haswa katika masuala ya kikodi ili kusaidia maendeleo ya nchi hizo mbili.

> *Tunatazamia Ushirikiano wa mafunzo haswa kwenye masuala ya kodi, na sehemu ambazo nchi zetu hizi mbili zina utaalamu mahsusi, lengo ni kujengeana uwezo pamoja ili tuweze kunufaika zaidi" alisema Dkt. Nchemba.*

Naye Balozi wa Oman nchini Tanzania, Mhe. Saud Al-Shidhani, ameipongeza Tanzania kwa kupiga hatua katika masuala ya kodi na ameona fursa ya kubadilisha uwezo katika masuala ya kodi ikiwa ni moja ya ajenda kubwa ya ushirikiano baina ya nchi hizo.

Mhe. Balozi Al-Shidhani, alisema kuwa biashara kati ya nchi hizi mbili umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kuna tija kubwa ya kuondoa Utozaji kodi mara mbili kwa wawekezaji na wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao kati ya nchi hizo mbili.















# MHE. CHANDE AZISHAURI BENKI KUCHANGAMKIA FURSA ZA MASOKO NJE YA NCHI

*Na. Peter Haule na Josephine Majura*

Naibu waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), ameitaka Akiba Commercial Bank Plc (ACB) na Taasisi zingine za Fedha, kuendelea na jitihada za kuongeza wigo wa uwekezaji na masoko nje ya nchi ili kujiimarisha.

Mhe. Chande alitoa rai hiyo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank Plc (ACB), Bw. Silvest Arumasi, kuhusu fursa za maendeleo, Ofisini kwake, jijini Dodoma.

Alisema kuwa Sekta ya Benki nchini ikikua, itatoa fursa kwa Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia benki za ndani kuliko kulazimika kwenda kutafuta fedha kwenye benki za nje ambazo hazimnufaishi mwananchi kwa kiwango kikubwa.

Aidha, ameihakikishia Benki hiyo kuwa Serikali itaendelea kushirikiana nayo pamoja na Benki nyingine nchini kwa kuwa lengo la Serikali kupitia Wizara ya Fedha ni kuhakikisha sekta ya Benki inaimarika na kutoa mchango katika maendeleo ya nchi.

Alisema Tanzania imeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta ya kibenki katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo yamekuwa na mchango katika maendeleo ya sekta mbalimbali.

Ameipongeza Benki ya ACB kwa kuendelea kufanya jitihada za kujimarisha ili kutoa huduma bora kwa wateja wake na Tanzania kwa ujumla.

*Lengo la Serikali ni kuhakikisha inakuza sekta ya Benki hususani Benki za Ndani ili kuchochea maendeleo", alisema Mhe. Chande.*




Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank Plc (ACB), Bw. Silvest Arumasi, aliipongeza Serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara na akaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi.

Alisema kuwa Benki hiyo imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuwahudumia wajasiriamali wadogo lakini inaendelea na jitihada za kuwafikia watu wengi zaidi.



*Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), akiongoza Mkutano kati yake na Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank Plc (ACB), Bw. Silvest Arumasi, Ofisini kwake, jijini Dodoma*



*Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), akiagana na Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank Plc (ACB), Bw. Silvest Arumasi, baada ya mazungumzo kuhusu maendeleo ya sekta ya Benki.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Akiba Commercial Bank Plc (ACB), Bw. Silvest Arumasi, akiipongeza Serikali kwa kuweka mazingira bora ya kufanyia biashara, wakati wa mazungumzo na Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), jijini Dodoma.*



# UINGEREZA KUISAIDIA TANZANIA KUENDELEZA SEKTA YA AFYA

*Na. Joseph Mahumi*

Tanzania na Uingereza zimesaini hati za Makubaliano ya nyongeza ya kuchangia Mfuko wa Kusaidia Sekta ya Afya (Health Basket Fund (HBF) kati ya Serikali na wadau wa maendeleo (Development Partners) ya pauni milioni 10 (sawa na Tsh bilioni 34), itakaowezesha utoaji wa huduma bora za afya nchini kuanzia mwaka 2024 hadi 2029.

Hati hizo zilisainiwa jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John A. Jingu, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Grace E. Magembe na Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, Bi. Olukemi Williams, hafla iliofanyika katika ukumbi wa ofisi za Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Akizungumza baada ya kusaini hati hizo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alisema kuwa Serikali inafuraha kusaini nyongeza ya makubaliano ya awali na sasa Serikali ya Uingereza itatambuliwa kama mmoja wa Washirika wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Kusaidia Sekta ya Afya kwa mujibu wa makubaliano ya awali (MoU) kati ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo yaliyosainiwa Julai 2021.



*Lengo la Mfuko wa kusaidia Sekta ya Afya ni kuunganisha rasilimali za kifedha ili kuboresha huduma za afya nchini Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo mbalimbali ikiwemo Serikali za Jamhuri ya Ireland, Denmark, Uswisi, KOICA, UNFPA na UNICEF, ili kuhakikisha kuwa tunafikia malengo ya kuboresha huduma za afya nchini", alisema Dkt. Mwamba*

Dkt. Mwamba aliongeza kuwa Mchango wa Mfuko wa kusaidia Sekta ya Afya umeleta mabadiliko makubwa katika huduma za afya nchini, kwani imeendelea kupunguza viwango vya vifo vya watoto na kuongeza upatikanaji wa huduma za msingi za afya katika ngazi ya jamii.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, amesema kuwa mfuko wa Afya, tayari umesaidia huduma za afya katika hospitali za wilaya, vijiji, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1999.

*Tumekubaliana kwa miaka mitano wanatupa pauni milioni 10 (sawa na Tsh bilioni 34) ambazo zitaenda kwenye mfuko wa kusaidia Sekta ya Afya, na tunapoungwa mkono na wadau wetu hawa ni jambo zuri" alisema Dkt. Jingu*



Kwa upande wa Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, Bi. Kemi Williams, amesema kuwa Serikali ya Uingereza inafahamu umuhimu wa kufikia huduma za afya kwa wote na kuna haja ya kuwa na mifumo ya afya imara na inayoweza kuhimili changamoto kwa njia ya kushirikiana.



*Huduma za afya kwa wote maana yake ni kuwa watu wote, popote walipo au wanapoishi, wanapata huduma bora za afya wanapozihitaji na mahali zinapohitajika bila kuangalia hali zao za kifedha" alisema Bi. Williams*

Aliongeza kuwa Serikali ya Uingereza inatambua na kupongeza jitihada za kiwango cha juu za Serikali ya Tanzania chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kufanikisha huduma za afya kwa wote, kama inavyoonekana kupitia mageuzi yanayoendelea katika upanuzi wa huduma za msingi za afya na utekelezaji wa sera ya bima ya afya kwa wote.



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (wa pili kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu (wa kwanza kushoto), Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Grace Magembe (wa kwanza kulia) na Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, Bi. Kemi Williams (wa pili kulia), wakionesha hati za Makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Uingereza ya nyongeza ya pauni milioni 10 (sawa na Tsh bilioni 34), ya kuchangia Mfuko wa Kusaidia ya Sekta ya Afya (Health Basket Fund (HBF) itakaowezesha utoaji wa huduma bora za afya nchini kuanzia mwaka 2024 hadi 2029.*



# TANZANIA NA HUNGARY KUENDELEZA USHIRIKIANO KATIKA MAENDELEO NCHINI

*Na. Benny Mwaipaja*

Balozi wa Hungary hapa nchini mwenye Makazi yake Jijini Nairobi nchini Kenya, Mhe. Zsolt Mészáros, ameipongeza Tanzania kwa kusimamia vema sera zake za fedha na uchumi, hatua iliyoifanya iendelee kuimarika kiuchumi na kuahidi kuwa nchi yake itaongeza ushirikiano kwa faida ya nchi hizo mbili.

Mhe. Mészáros aliyasema hayo katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa nchi yake imekuwa ikifuatilia kwa karibu maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania ikiwemo hatua kubwa inazochukua kuvutia uwekezaji wakiwemo wanaotoka nchini mwake.

Aliahidi kuwa nchi yake iko tayari kushirikiana na Tanzania katika kuchangia maendeleo yake hususan katika sekta za huduma za jamii kama vile maji kupitia mpango wake maalumu wa kushirikiana na Serikali ujulikanao kama Tied Aid Facility.

Akizungumza na Balozi huyo wa Hungary, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) amesema kuwa uchumi wa Tanzania umeimarika ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, uchumi umekua kwa wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Alisema kuwa makadirio ya ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2024/2025 ni wastani wa asilimia 5.4 na asilimia 5.8 mtawalia, kufuatia miongozo na usimamizi mzuri wa uchumi, wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwezi Agosti mwaka 2024, zinaonesha kuwa uchumi wetu umeimarika licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali huku ukuaji huo ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za ujenzi, kilimo, fedha na sekta ya bima" alisema Dkt. Nchemba.*



*Balozi wa Hungary nchini, mwenye Makazi yake Jijini Nairobi nchini Kenya, Mhe. Zsolt Mészáros, akizungumza wakati wa kikao chake na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akizungumza wakati wa kikao chake na Balozi wa Hungary nchini, mwenye makazi yake Jijini Nairobi nchini Kenya, Mhe. Zsolt Mészáros, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam.*

Aidha, Dkt. Nchemba alimweleza Balozi huyo kuwa kasi ya mfumuko wa bei imedhibitiwa na kuwa katika kiwango cha asilimia 3.1 na kuwa katika wigo wa tarakimu moja, kiwango kilichokubaliwa pia katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zilizoweka ukomo wa asilimia 8 na kiwango cha nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) cha asilimia 3 hadi 7.

Alisema kuwa uimara wa uchumi wa Tanzania umethibitishwa pia na mashirika yanayofanya tathimni ya hali ya uchumi wa nchi mbalimbali duniani ikiwemo Taasisi ya Moody's ambayo hivi karibuni, iliipandisha Daraja Tanzania kutoka Daraja B2 kwenda Daraja B1 pamoja na Taasisi ya Fitch ambayo imeipa Tanzania Daraja la B+ yenye Mtazamo Chanya (positive Outlook).

Dkt. Nchemba alisema kuwa hatua hiyo imeifanya Tanzania na sekta binafsi kuaminiwa zaidi na taasisi za fedha za kimataifa kwamba zinaweza kuyafikia masoko ya fedha ya kimataifa na kuvutia uwekezaji wa mitaji na teknolojia kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Alitoa wito kwa wawekezaji kutoka Hungary kuja kuwekeza nchini katika maeneo balimbali watakayoona yanawafaa kutokana na Serikali kuweka mazingira bora yanayovutia uwekezaji.





# WAHASIBU WANAWAKE WATAKIWA KUSIMAMIA VEMA FEDHA ZA UMMA

*Na. Farida Ramadhani*

Wahasibu wanawake nchini wametakiwa kusimamia vizuri fedha za umma katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Wito huo ulitolewa jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo kwa niaba ya Katibu Mkuu, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, katika ufunguzi wa mafunzo kwa Wahasibu Wanawake kutoka kwenye Mafungu na Halmashauri.

Bi. Omolo alisema Serikali inatarajia wahasibu hao watazingatia mafunzo yanayotolewa ili kuleta tija na kufikia lengo la Serikali la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.

Alisema katika mafunzo hayo wahasibu watajifunza kuhusu mawasiliano, masuala ya fedha na uwezeshaji wa kiuchumi, usimamizi wa wakati, namna ya utatuzi wa matatizo na maadili pamoja na afya ya akili.

*Mafunzo haya yatawaongezea uwezo mzuri katika mawasiliano kwa maandishi, mawasiliano ya kibinafsi na majadiliano kwa kukuza ujuzi wa kusikiliza na kuelewa mitazamo ya wengine. ujuzi wa mawasiliano kwa wanawake wahasibu itasaidia kujenga uhusiano mzuri, kukuza uwazi na mshikamano na kutatua migogoro mahali pa kazi na kwenye jamii", alibainisha Bi. Omolo.*



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, akifungua kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, mafunzo kwa Wahasibu Wanawake kutoka kwenye Mafungu na Halmashauri ili kuwajengea uwezo wa usimamizi wa fedha za umma yaliyofanyika jijini Dodoma.*



Bi. Omolo alisema elimu hiyo itawafanya wahasibu hao wawe na ujuzi stahiki wa usimamizi wa kifedha binafsi, kupangilia bajeti na matumizi, kuona fursa za uwekezaji na namna ya kuzitumia.

Kwa upande wake, Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi Bw. Ayoub Banzi kwa niaba ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bw. Leonard Mkude, alisema mafunzo hayo yatatolewa kwa wahasibu wanawake takribani 300 ambao ni sehemu ya wahasibu wanawake kutoka Mafungu na Halmashauri zote za Tanzania Bara.

Alisema mafunzo hayo ni ya kwanza kutokewa katika mafunzo mengi ambayo wanatarajia kufanya ili kuendeleza na kuunga mkono juhudi za kumnyanyua na kumuwezesha mwanamke.



*Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi, Bw. Ayoub Banzi, akizungumza kwa niaba ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bw. Leonard Mkude, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Wahasibu Wanawake kutoka kwenye Mafungu na Halmashauri ili kuwajengea uwezo wa usimamizi wa fedha za umma.*



# DKT. MWAMBA AISHUKURU ITALIA KWA KUCHANGIA MAENDELEO YA TANZANIA

*Na. Benny Mwaipaja*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, ameushukuru Umoja wa Ulaya kwa mchango wake katika maendeleo ya nchi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayofadhiliwa na Umoja huo na kuongeza kuwa Serikali iko tayari kuendeleza ushirikiano huo kwa faida ya pande zote mbili.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, akisalimiana na Mkuu wa Masuala ya Ushirikiano wa Umoja wa Ulaya nchini, Bw. Marc Stalmans, alieongoza Timu ya Wataalamu kutoka Umoja wa Ulaya jijini Dodoma.*

Dkt. Mwamba ametoa shukrani hizo alipokutana na kufanya mazungumzo na Timu ya Wataalamu kutoka Ofisi za Ubalozi wa Umoja wa Ulaya nchini, iliyoongozwa na Mkuu wa Ushirikiano wa Umoja huo hapa nchini, Bw. Marc Stalmans, katika Ofisi za Hazina-Jijini Dodoma.

Pamoja na Mambo mengine, wataalam hao walitoa taarifa fupi ya utekelezaji wa awamu ya kwanza kwa miaka minne (4) ambao umetekelezwa kwa mafanikio makubwa, ambapo jumla ya EURO 366 Millioni (sawa na trilioni 1.075 za kitanzania) zimetengwa kwenye miradi 6 ya kitaifa na EURO 141 Milioni (sawa bilioni 414.17 za kitanzania) zimetengwa kwenye miradi ya kikanda inayoendelea.



Dkt. Mwamba alisema kuwa Umoja wa Ulaya umekuwa mstari wa mbele kuwekeza kwenye miradi muhimu kwa maisha ya watu na uchumi wa nchi na kueleza kuridhika kwake na mipango mipya ya ushirikiano inayotekelezwa na pande hizo mbili ikiwemo kuendeleza sekta za kilimo.

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika kikao hicho ni tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele vya ushirikiano vilivyokubalika katika kipindi cha Miaka 7 kuanzia mwaka 2021 hadi 2027, ikiwemo Mpango wa kijani, Mtaji wa Watu na Ajira na Utawala bora, maarufu kama Multi-annual Indicative Programme 2021-2027.

Kwa upande wake Mkuu wa Ushirikiano wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Bw. Marc Stalmans, alisema ushirikiano kati ya Umoja huo na Tanzania umekuwa wa kupigiwa mfano katika Bara la Afrika na kuahidi kuendeleza ushirikiano huo kwa manufaa ya pande zote mbili.

Alitoa pongezi kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kwa kuweka mipango bora inayochochea maendeleo ya watu ikiwemo kuboresha mazingira ya ufanyajibiashara na ufanisi wa sekta binafsi hatua inayochangia kusisimua na kuchochea maendeleo ya nchi.

Hadi sasa Umoja wa Ulaya umeidhinisha utekelezaji wa awamu ya pili wa mpango huo ambapo kiasi cha EURO 219 Millioni (sawa bilioni 641.95 za kitanzania) zitaelekezwa kwenye vipaumbele vya awali pamoja na Miradi inayohusu Malighafi Muhimu (Critical Raw Materials).

Kikao hicho kilihudhuriwa na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Fedha za Nje, Bw. James Msina, Mkuu wa Masuala ya Msaada kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya, Kitengo cha Uratibu na Ushirikiano, Bw. Jonathan Mpuya, Mkuu wa Fedha na Utawala - Kitengo cha Uratibu na Ushirikiano, Bw. Ibrahim Muhazi, Afisa wa Mpango wa Rasilimali Asili, Bw. Leonard Lema, na maafisa wengine kutoka Umoja wa Ulaya nchini.







# SERIKALI YASISITIZA TAFITI ILI KUIMARISHA UCHUMI

*Na. Josephine Majura na Saidina Msangi*

Serikali imetoa rai kwa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kufanya tafiti za bidhaa za mazao ya uvuvi, hususani kwa upande wa Ziwa Victoria ambalo kwa sehemu kubwa linagusa wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa ili kuibua miradi ya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bw. Elijah Mwandumbya kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb,) kwenye sherehe za Mahafali ya 38 ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, duru ya pili Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa, Kisesa mkoani Mwanza yanayofanyika kwa mara ya 12 katika Kituo hicho.

Alisema Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wavuvi na wafugaji wa samaki ili waongeze uzalishaji, kuzalisha ajira, kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza kipato cha wavuvi na watu waliopo kwenye mnyororo wa thamani na hivyo kuchangia kwenye Pato la Taifa.

*Eneo linalopewa uzito wa hali ya juu na Serikali ni pamoja na elimu biashara, ufugaji wa nyuki, uvuvi, ufugaji wa mifugo, kilimo cha mazao ya nafaka pamoja na uongezaji wa thamani ya bidhaa ikiwemo bidhaa za uvuvi, kilimo, mifugo pamoja na madini", alisema Bw. Mwandumbya.*



Aidha, Bw. Mwandumbya aliuagiza Uongozi wa Chuo kuangazia sekta ya madini hasa ikizingatiwa kuwa ukuaji wa sekta hiyo umeongezeka na kuajiri vijana wengi ambapo kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inakadiriwa mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa utaongezeka na kufikia asilimia 10 au zaidi kufikia Mwaka 2025.

Alisisitiza kuwa eneo la madini ni eneo ambalo Chuo kinapaswa kuliangalia kwa jicho la aina yake na kushiriki kuchagiza uchumi wa Taifa kupitia tafiti endelevu na shirikishi za uongezaji wa thamani ya madini.

Alilipongeza Baraza la Uongozi wa Chuo kwa kuendelea kukisimamia vyema Chuo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo fursa ya kuitumikia jamii kupitia miradi mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inayogusa watu wa chini katika jitihada za kuwainua kiuchumi, hususan katika sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Akizungumza na wahitimu Bw. Mwandumbya alisema kuwa ana imani kuwa ujuzi walioupata watautumia katika kuleta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za maendeleo zinazoikabili jamii.

Alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuweka mazingira mazuri ya kujiajiri, hususan kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na hivyo kuongeza fursa za vijana wakiwemo wasomi kujiajiri na hatimaye kupunguza tatizo la ajira.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Prof. Hozen Mayaya, alisema kuwa Chuo kimejizatiti katika kuandaa wataalamu wenye weledi wa kutosha katika fani za mipango ya maendeleo, kujenga moyo wa uzalendo na uadilifu kwa wataalamu hao ambazo ni nyenzo za msingi wa maendeleo na ustawi wa nchi.

Aidha, alisisitiza kuwa Chuo kitaendelea kufuata kanuni zote za matumizi ya fedha ya umma ili thamani ya fedha ionekane.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo CPA. Dkt. Samwel Werema, alisema kuwa Chuo kinatarajia kuendela na ujenzi wa miundombinu katika Kampasi zote mbili za Dodoma na Mwanza ili kupunguza tatizo la mabweni kwa wanafunzi.



*Chuo kitaendelea kuboresha mahusiano na wadau wa ndani na nje ili kuwa na ushirikiano thabiti na wa kudumu katika kazi za ushauri elekezi, mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na tafiti", alisema CPA. Dkt. Samwel Werema.*

Aidha, alisisitiza kuwa Chuo kitaendelea kuhuisha mitaala ili kuendana na mahitaji ya soko pamoja na kuboresha shughuli za ushauri elekezi ili kutoa huduma bora inayokidhi mahitaji ya soko kwa wadau.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa Mwanza, Prof. Juvenal Nkonoki, alisema kuwa katika Mahafali hayo kulikuwa na jumla ya wahitimu 2,545 wanaume 1,156 na wanawake 1389 ikiwa ni ongezeko mara kumi ya idadi ya wahitimu wa Mahafali yaloiyofanyika kwa mara ya kwanza mwaka



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, akimtunuku mwanafunzi pekee aliyehitimu Shahada ya Uzamili ya Mipango Ufutiliaji na Tathmini Bw. Joseph Ochora, katika Mahafali ya 38 ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, duru ya pili Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa, Kisesa Mwanza, yaliyofanyika kwa mara ya 12 katika Kituo hicho.*

# WAWEKEZAJI KUTOKA ITALIA NA FURSA YA KUKUZA AJIRA NA UCHUMI TANZANIA

*Na. Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ametoa wito kwa wawekezaji kutoka nchini Italia kutumia mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo hapa nchini kuwekeza mitaji yao katika miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ili kukuza uchumi wa pande hizo mbili.

Dkt. Nchemba alitoa wito huo alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Italia hapa nchini Mhe. Giussepe Sean Coppola, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka vivutio mbalimbali vya uwekezaji na kuialika sekta binafsi ya Italia, kushirikiana na Serikali kwa kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa miradi mbalimbali hapa nchini ukiwemo mradi wa Reli ya Kisasa wa SGR.

Kwa upande wake, Balozi wa Italia hapa nchini Mhe. Giussepe Sean Coppola, alimwagia sifa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia vizuri uchumi na maendeleo ya nchi ikiwemo kuunda tume ya kushughulikia changamoto za kikodi nchini.



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (kushoto), akiwa na Balozi wa Italia nchini, Mhe. Giussepe Sean Coppola, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam.



Alisema kuwa anaamini matokeo ya Tume hiyo yataongeza chachu ya kufanyabiashara na uwekezaji hapa nchini hatua itakayochochea ajira, ukuaji wa uchumi na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kuchochea maendeleo ya nchi.

Aliahidi kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika Nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa kuchangia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo kwa kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la kahawa chini.

Uhusiano kati ya Tanzania na Italia ulianza rasmi tarehe 9 Desemba 1961, wakati Italia ilipoanzisha ubalozi wake mjini Dar es Salaam, ambapo Uhusiano huo umejikita katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na biashara, maendeleo, elimu, na ushirikiano wa kijamii. Italia imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo wa Tanzania kwa kufadhili miradi mbalimbali kupitia bajeti kuu ya Serikali, ikiwemo miradi ya maji, afya, mafunzo ya ufundi stadi na huduma katika sekta za utalii na hoteli, kilimo, uchumi wa buluu, mazingira na usawa wa kijinsia.



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (katikati) na Balozi wa Italia nchini, Mhe. Giuseppe Sean Coppola (wa tatu kulia), wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumalizika kwa kikao chao kilichofanyika katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam, Wengine katika picha ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (wa tatu kushoto), na Maafisa wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.*





# SERIKALI YAISHUKURU CHINA KWA USHIRIKIANO KATIKA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA SGR

*Na. Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameishukuru China kwa kufikia hatua za mwisho za kufadhili ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR unaendelea hivi sasa kwa kipande cha tano cha kuanzia Mwanza hadi Isaka na kuahidi kuyafanyiakazi maombi mengine ya kipande cha sita kinachoanzia Tabora hadi Kigoma.

Dkt. Nchemba aliyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa China hapa nchini, Mheshimiwa Chen Mingjian, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam, ambapo walijadili masuala muhimu ya ushirikiano kati ya China na Tanzania uliodumu kwa miaka 60 sasa.



Dkt. Nchemba alisema kuwa Mradi wa Reli ya Kisasa ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya Watanzania na kwamba ujumbe wa Mheshimiwa Balozi Chen kwamba China kupitia taasisi zake inakamilisha taratibu za ndani za kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo umepokelewa kwa mikono miwili na Serikali.

Kwa upande wake, Balozi wa China hapa nchini, Mheshimiwa Chen Mingjian, alisema kuwa nchi yake inauchukulia uhusiano wake na Tanzania kuwa ni wa kipekee na kwamba maelekezo ya Kiongozi wa nchi hiyo Mheshimiwa XI Jinping ni kwamba anataka uhusiano huo uwe wa mfano na kielelezo barani Afrika.

Alisisitiza kuwa maombi ya Tanzania ya kupata fedha kwa ajili ya kipande cha tano na mengine ya kutaka ufadhili wa ujenzi wa kipande cha 6 yamepokelewa na kwamba uamuzi wake utatolewa hivi karibu baada ya mambo machache yanayofanyiwakazi kukamilika.

Aidha, alieleza kuwa mpango wa miaka mitatu wa China wa ushirikiano kati yake na nchi za Afrika (FOCAC), umeitengea Tanzania kiasi kikubwa cha fedha ambazo zitaelekezwa katika miradi inayogusa masuala ya uchumi wa kijani, biashara na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT).

# JAPAN YAISAIDIA TANZANIA SH.BILIONI 68.5 KUJENGA BARABARA ZA MZUNGUKO JIJINI DODOMA



*Na. Farida Ramadhani*

Japan, kupitia Shirika lake la Ushirikiano wa Kimataifa (JICA), imeipatia Tanzania msaada wa Yen bilioni 4.07 sawa na shilingi bilioni 68.5 za Tanzania kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa Barabara ya mzunguko wa ndani katika Jiji la Dodoma.

Mkataba wa Msaada huo ulitiwa Saini katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba kwa upande wa Tanzania, Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Yasushi Misawa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Hitoshi Ara.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alisema kuwa Mradi huo utahusisha upanuzi wa barabara kutoka njia mbili hadi nne kuanzia mzunguko wa barabara ya Bahi hadi Image na ujenzi wa barabara mpya ya njia nne kuanzia mzunguko wa barabara ya Image hadi mzunguko wa barabara ya Makulu.

*"Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mzunguko wa Ndani ya Jiji la Dodoma, unaendana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22– 2025/26) wenye maudhui ya kufikia ushindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu ambao unalenga kuongeza ufanisi na uzalishaji kwa kutumia rasilimali zilizopo" alisema Dkt. Mwamba*



*Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Balozi wa Japan nchini Tanzania Mhe. Yasushi Misawa wakisaini mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 68.5 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara za mzunguko za ndani za jiji la Dodoma, katika hafla ilyofanyika jijini Dar es Salaam.*

Dkt. Mwamba alisema mikataba hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano imara kati ya Tanzania na Japan ambapo Tanzania imenufaika na ufadhili wa Japan kwa njia ya misaada na mikopo nafuu katika maeneo ya sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, maji, afya, nishati, usafirishaji na maendeleo ya miji, usimamizi bora wa fedha za umma pamoja na elimu.

Kwa upande wao, Balozi wa Japan Nchini Tanzania, Mhe. Yashushi Misawa na Mwakilishi Mkazi wa (JICA), Bw. Hitoshi Ara, walisema kuwa mradi huo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kwa kuwa



*Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Mwakilishi Mkazi wa (JICA), Bw. Hitoshi Ara wakibadilishana mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 68.5 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara za mzunguko za ndani za jiji la Dodoma.*

Dodoma ni Jiji ambalo lipo katika korido ya katikati ambayo inazidi kuwa muhimu kama njia kuu ya uchumi unaokua kwa kasi Afrika Mashariki.

Walisema kupitia mkataba hiyo Japani itajenga takribani kilomita 3.1 za Barabara ya mzunguko na kupanua takribani kilomita 3.4 za Barabara ndani ya Jiji la Dodoma ambazo zitasaidia kuzuia magari makubwa kuingia mjini ili kukabiliana na athari za kimazingira.
Waliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania na kubaninisha kuwa mikataba hiyo ni ishara tosha ya uhusiano mzuri uliopo kati yq nchi hizo mbili.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Dkt. Charles Msonde , alisema Wizara hiyo itasimamia kikamilifu fedha hizo na kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kama ilivyopangwa.

Alisema kuwa mradi huo unatarajiwa kutatua changamoto mbalimbali za miundombinu katika Jiji la Dodoma kwa kuwa baada ya Serikali kuhamia katika Jiji hilo mahitaji ya miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara yameongezeka.

Alitaja baadhi miradi iliyotekelezwa kwa kushirikiana na Japan ikiwemo Daraja la Gerezani, upanuzi wa Barabara ya Bagamoyo pamoja na ujenzi wa Daraja la Rusumo.




# MHE. CHANDE AIPONGEZA TIA KWA KUFANIKISHA MBIO ZA MARATHON

*Na. Scola Malinga*

Naibu waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb) ameipongeza Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) kwa kuandaa mbio za marathon kwa lengo la kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu na kuitangaza Taasisi.

Mhe. Chande alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati wa kilele cha TIA marathon 2024 ambapo alikuwa mgeni rasmi.

> *Michezo ikiwemo riadha ni nyenzo muhimu ya kuunganisha watu na kujenga umoja, napenda kuipongeza TIA na wadau wengine kwa kuwezesha jambo hili kufanikiwa ikiwa ni pamoja kushirikisha wadau mbalimbali", alisema Mhe. Chande.*

Alisema kuwa michezo inadumisha umoja lakini pia inatoa mwanga kwa vijana wanaopenda michezo na kuimarisha mwili.

Aidha amesema kuwa TIA inatekeleza Sera ya Taifa ya maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 ya kuhamasisha wananchi kushiriki michezo na mazoezi ya viungo vya mwili ili kuimarisha afya zao.

Mhe. Chande alisema kuwa pia ibara ya 242 na 243 (c) za Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, CCM 2020-2025, michezo imepewa kipaumbele kikubwa kwa kuwa ni fursa ya ajira, burudani, afya na inawajengea umoja wananchi.

> *"Kipekee kabisa ninajivunia sana kuona tukio hili likiandaliwa na TIA, taasisi iliyo chini ya wizara ninayoiongoza kwa kauli mbiu yenye nguvu "Run, Inspire, and Support", alieleza Mhe. Chande.*

# KONGAMANO LA KODI LAFANYIKA JIJINI DODOMA

*Na. Eva Ngowi*



Serikali kupitia Wizara ya Fedha imefanya kongamano la kodi kikanda kwa kuwakutanisha Wadau kutoka sekta binafsi wakijumuisha wataalam na washauri wa kodi, wadau wa sekta mbalimbali nchini, wafanyabiashara, wazalishaji wa bidhaa na mazao mbalimbali pamoja na Makundi Maalum ili kuboresha mifumo ya kodi itakayochochea mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

Hayo yalielezwa na Kamishna Msaidizi Idara ya Sera Bw. William Mhoja, katika kongamano la kwanza la kodi kikanda kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, lililofanyika jijini Dodoma.

Bw. Mhoja alisema kongamano hilo litasaidia kuboresha uratibu wa ukusanyaji maoni na kuongeza ushirikishwaji wa makundi mbalimbali katika uaandaji wa bajeti ya Serikali na utunzi wa sheria.



*Hatua hii ni moja ya utamaduni wa kutambua mchango wa wananchi kupitia kodi, ada na tozo mbalimbali ambazo zinawezesha ujenzi wa Taifa letu" Alisema Bw. Mhoja.*

Alisema kuwa lengo la kongamano hilo lilikuwa kupata maoni mbalimbali kwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na kupita kwenye Kanda ikiwemo Kanda ya Dodoma ambayo ukusanyaji maoni umenza, Arusha, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Iringa na baadae Mtwara na kuhitimisha zoezi hilo Dar es Salaam.

Alisema kuwa katika kongamano hilo maoni yote yatakayotolewa na wadau mbalimbali yatafanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kuyafanyia utafiti kabla ya kufanyiwa utekelezaji.



*Kamishna Msaidizi Idara ya Sera, Wizara ya Fedha, Bw. Juma Mkabakuli (wa kwanza kushoto) akiwa na Kamishna Msaidizi Idara ya Sera, Wizara ya Fedha Bw. William Mhoja wakisikiliza maoni mbalimbali yanayotolewa na wataalam na washauri wa kodi, wadau wa sekta mbalimbali nchini, wafanyabiashara, wazalishaji wa bidhaa na mazao mbalimbali katika Kongamano la Kodi lililofanyika jijini Dodoma.*

*Hivyo Serikali inawaahidi kwamba maoni yao yanazingatiwa sana kama ambavyo mmeona katika Hotuba za bajeti na Serikali inawakaribisha sana kushiriki na kutoa maoni. Kimsingi maoni ya wananchi wote yanazingatiwa na nawaomba sana wananchi wote wajitokeze kutoa maoni na maoni yao yatafanyiwa kazi kwa sababu mengine yanahitaji kufanyiwa utafiti kwanza kabla ya kuyaleta kwenye utekelezaji" alisema Bw. Mhoja.*

Aidha, aliwashukuru Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) pamoja na TradeMark Afrika kwa kushirikiana na Serikali hususan katika kudhamini baadhi ya shughuli mbalimbali katika makongamano haya.



*Kamishna Msaidizi Idara ya Sera, Wizara ya Fedha Bw. William Mhoja (wa kwanza kulia walioketi), akiwa katika picha ya pamoja na wataalam na washauri wa kodi, wadau wa sekta mbalimbali nchini, wafanyabiashara, wazalishaji wa bidhaa na mazao mbalimbali, (wa kwanza kushoto ni Kamishna Msaidizi Idara ya Sera, Wizara ya Fedha Bw. Juma Mkabakuli, katika Kongamano la Kodi lililofanyika jijini Dodoma.*

Kwa upande wa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania Bw. Alexander Malya, aliwaasa wafanyabiashara kote nchini watoe maoni yao kuhusiana na masuala mazima ya mapendekezo ya mabadiliko ya kodi.



*Kwa niaba ya Jumuiya ya Wafanyabiashara tunawahamasisha wafanyabiashara wa mikoa yote Tanzania kushiriki makongamano haya yatakapowafikia kwenye Kanda zao, kwenye mikoa yao kushiriki kikamilifu na kutoa maoni yao kuhusu suala zima la mapendekezo ya mabadiliko ya kodi", Alisema Bw. Malya*

Kongamano hili ni mwendelezo wa Kongamano la Kodi Kikanda lililoanzishwa na Wizara ya Fedha mwezi Novemba mwaka 2023 ambapo vikao vilifanyika Kikanda katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Shinyanga, Kigoma, Lindi na Mtwara.



# SERIKALI KUONGEZA BAJETI YA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI

*Na. Saidina Msangi na Ramadhani Kissimba*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) amesema Serikali itaendelea kukiwezesha kibajeti Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) ili kiweze kuwa na miundombinu na rasilimali watu inayokidhi mahitaji ya utoaji wa elimu kwa viwango bora.

Akizungumza kwa niaba ya Mhe. Dkt. Nchemba katika Mahafali ya 38 duru ya kwanza yaliyofanyika katika Kampasi Kuu ya Dodoma, Kamishina wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja alisema ili kuboresha sekta ya elimu nchini Serikali inakusudia kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Dkt. Mwamwaja alisema kuwa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa muda mrefu kimekuwa kikipitia kwenye mafanikio makubwa kutokana na mikakati iliyojiwekea hasa ile ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia program mbalimbali ikiwemo uanzishwaji wa Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu (Mipango Enterprenurship and Innovation Centre - (MEI)), pamoja na miradi inayoendeshwa na wabia wa maendeleo wakiwemo Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Programme – UNDP).

Alitumia Mahafali hayo kuushauri Uongozi wa Chuo kupanua wigo wa miradi katika upande wa miradi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili huduma hiyo iwafikie wananchi wengi zaidi na waweze kunufaika na fursa zinazotokana na huduma hizo.

*Aidha, kwa upande wa miradi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ninawashauri kupanua wigo wa maeneo mengine ya nchi ili wananachi wengi zaidi wanufaike na huduma zenu na kwa kufanya hivyo mtawasaidia kujikwamua kiuchumi'' aliongeza Dkt. Mwamwaja.*




Dkt. Mwamwaja kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe.Dkt.Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) aliwataka wahitimu na wananchi kwa ujumla kujitokeza na kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za mitaa utakaofanyika tarehe 27 Novemba,2024,Uchaguzi ambao ni muhimu katika kuimarisha demokrasia na ushiriki wa wananchi katika utawala wa nchi yao.

Awali, akiongea katika Mahafali hayo, Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Profesa Hozen Mayaya, alisema Chuo hicho kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya Kitaaluma kwa mafanikio makubwa ambapo inajivunia kutoa wahitimu waliopata mafunzo ya darasani na mafunzo kwa vitendo jambo ambalo litawajengea umahiri katika nyanja walizosomea.

Aidha, Profesa Mayaya, alisema kuwa pamoja na kuadhimisha Mahafali ya 38, Chuo pia kinatimiza miaka 45 tangu kuanzishwa na kwa kipindi chote hicho Chuo kimepitia mafanikio mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo wahadhiri wa chuo katika kufanya utafiti, kutekeleza miradi mbalimbali ya tafiti shirikishi kwa lengo la kujenga uwezo kwa Taasisi na Wadau.



*Ninapenda kukutaarifu kuwa katika azma yake ya kuwajengea uwezo wahadhiri katika kufanya utafiti, Chuo kimendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya tafiti ambazo zinalenga katika kutatua changamoto za kiuchumi zinazoikabili jamii na Taifa kwa ujumla'' alisema Prof. Mayaya.*

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo Profesa Joseph Kuzilwa alisema kuwa jukumu mojawapo la Baraza la Uongozi wa Chuo ni kuendelea kukisimamia Chuo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuzingatia thamani ya fedha.

Profesa Kuzilwa aliongeza kuwa mafanikio makubwa yanayopatikana Chuo cha Mipango ni kutokana na kuwa na Viongozi wenye weledi mkubwa katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Chuo kwa kuzingatia sheria na Baraza la Chuo litaendelea kuhakikisha Chuo kinatekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria, taratibu, kanuni na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Mahafali ya 38 duru ya kwanza ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini yamejumuisha wahitimu 5,589 kutoka katika programu mbalimbali kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada ya Umahiri ambapo kati yao wanaume ni 2,455 na wanawake 3,134.




*Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt.Charles Mwamwaja, akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wahadhili wa Chuo cha Mipango, baada ya kuhitimisha kutunuku shahada mbalimbali kwa wahitimu katika Mahafali ya 38 duru ya kwanza ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere Kampasi Kuu ya Dodoma, jijini Dodoma.*

# BENKI YA DUNIA YAIPATIA TANZANIA SH. BILIONI 248 KUSAIDIA MAENDELEO YA WANAWAKE NA KUKABILIANA NA UKATILI WA KIJINSIA



*Na Farida Ramadhani na Chedaiwe Msuya*

Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia (WB) wamesaini mikataba miwili (2) yenye thamani ya dola za Marekani milioni 104, sawa na takriban shilingi bilioni 248, kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia nchini Tanzania, maarufu kama "PAMOJA".

Hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo imefanyika jijini Dar es Salam kati ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa niaba ya Serikali na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bw. Nathan Belete.

Akifafanua kuhusu mikataba hiyo, Mhe. Dkt. Nchemba alisema kuwa mkataba wa dola za Marekani milioni 4, sawa na zaidi ya shilingi bilioni 9.5 ni msaada na Mkataba wa dola za Marekani milioni 100, sawa na zaidi ya shilingi bilioni 238 ni mkopo wenye masharti nafuu.

Alisema mradi wa PAMOJA uliosainiwa utasaidia kuongeza upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na huduma za kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia Tanzania Bara na Zanzibar.



*Hili litatimizwa kupitia uimarishaji vikundi vya wanawake kwa kuwajengea ujuzi wa biashara na kuwaunganisha na fursa za masoko, kuongeza fursa za mikopo nafuu kwa vikundi vya wanawake, kuwaongezea upatikanaji wa huduma za kifedha kupitia mifumo rasmi ya kifedha pamoja na kuimarisha huduma za kukabiliana na ukatili wa kijinsia", alifafanua Mhe. Dkt. Nchemba*

Alisema mradi huo utawanufaisha moja kwa moja wanawake wapatao 319,850 na walengwa wengine 399,000, wakiwemo wanafamilia za wanufaika.

Alisisitiza kuwa kukuza usawa wa kijinsia si suala la wanawake pekee bali ni msingi wa Taifa la kidemokrasia, lenye haki na linalostawi na kuongeza kuwa kuondoa tofauti za kijinsia kunaboresha uzalishaji na kuimarisha uhimilivu wa kiuchumi.

*Mradi wa PAMOJA ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa 2021/22 - 2025/26, Rasimu ya Dira ya Maendeleo ya 2050 na pia ni sehemu ya ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye amelipa kipaumbele suala la usawa wa kijinsia", alisema Mhe. Dkt. Nchemba.*

Alisema utekelezaji wa mradi huo ni ushahidi wa dhamira ya Serikaliya kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (hususan Lengo la 5) na kuonesha nia thabiti ya kufanikisha ukuaji wa uchumi unaowajumuisha wote.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania, Bw. Nathan Belete, alisema kuwa mradi huo utatatua changamoto za kijinsia za kijamii na kiuchumi kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi na kubainisha mila potofu ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia.



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), (kulia) na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia – Tanzania, Bw. Nathan Belete, wakibadilishana Hati ya Mikataba Miwili (2) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 104 (sawa na takribani sh. bilioni 248) kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania, maarufu kama "PAMOJA", katika hafla iliyofanyika katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, jijini Dar es Salaam.*

Aliiomba Serikali kuzikutanisha pamoja Wizara zote za kisekta zinazohusika katika utekelezaji wa mradi huo kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake na Watoto.

Alisema wanatarajia mradi huo utaanza kutekelezwa mapema na kuona matokeo ya utekelezaji pamoja na faida watakazo zipata walengwa wa mradi huo.

Kwa upande wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb), alimpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada mbalimbali anazofanya kuwainua wanawake kiuchumi ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi wa PAMOJA.

Alisema katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo, Wizara yake imeshazindua Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake pamoja na Mkakati wake ambao uwezeshaji wanawake kiuchumi ni miongoni mwa malengo yake.

Alisema mradi huo umekusudia kujenga nyumba salama 10 kwa ajili ya kuwahifadhi Watoto wanaokumbana na ukatili wa kijinsia pamoja na kujenga vituo 200 vya malezi salama na makuzi ambapo vituo 184 vitakuwa Tanzania Bara na 16 vitajengwa Zanzibar.



*Afisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii wamekuwa wakihangaika kupata ofisi za kufanyiakazi na kutoa huduma pamoja na vifaa kazi ikiwemo usafiri, sasa kwa kutumia fedha hizi watapata Ofisi 40 za maafisa Maendeleo ya Jamii na Ofisi 40 za Maafisa Ustawi wa Jamii", alifafanua Mhe. Dkt. Ngwajima.*

Alisema fedha hizo zitasaidia kuwachangamsha wanawake kiuchumi, kupata elimu ya kibiashara, mitaji pamoja na kufanya biashara wakiwa na uelewa mpana kwa sababu wataalam wamewezeshwa kuwafikia popote walipo.

Aliahidi kuhakikisha fedha hizo zitatumika kikamilifu kwenye mradi iliyokusudiwa na kuleta matokeo Chanya.

# TANZANIA NA JAPAN KUIMARISHA USHIRIKIANO

*Na. Saidina Msangi na Asia Singano*

Serikali imesema kuwa itaendelea kushirikiana na Japan huku ikitoa wito kwa kampuni za Japan kuja kuwekeza nchini katika maeneo mbalimbali katika sekta zenye maslahi ya nchi zote mbili ikiwa ni pamoja na kukuza uwekezaji binafsi.

Hayo yalisemwa jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alipokutana na kufanya maungumzo na Mkurugenzi Mkuu Kanda ya Afrika wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bw. Naoki Yanase.

Aliishukuru Serikali ya Japan kwa kuendelea kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kutoa wataalamu wanaofanikisha kutekeleza miradi kwa wakati na kwa viwango vya juu na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuboresha hali ya maisha ya watanzania.

Alisema kuwa Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano na Serikali ya Japan ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya Uboreshaji wa Barabara ya Arusha-Holili, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar Mjini, ujenzi wa barabara za mzunguko wa ndani katika jiji la Dodoma ambayo ipo katika utekelezaji.

*Tangu kuanzishwa kwa ushirikiano Mwaka 1960, Tanzania imenufaika kwa kiasi kikubwa na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Japan na hivyo kuifanya Tanzania kuwa mnufaika mkubwa katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema Bi. Omolo.*





*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu Afrika wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bi. Urano Sayaka, baada ya kufika kwa ajili ya mkutano, jijini Dodoma.*

Akizungumza kuhusu maendeleo ya uchumi, Bi. Omolo alisema kuwa sera madhubuti za Serikali zimewezesha uchumi wa Tanzania kuendelea kuimarika ikirekodi kasi ya ukuaji wa asilimia 5.3 katika robo ya pili ya 2024, ikilinganishwa na 4.7 asilimia katika kipindi sawia cha mwaka 2023.

Aidha, mfumuko wa bei Oktoba 2024, ulifikia asilimia 3.0 ambayo ni ndani ya lengo na pia ni ndani ya wigo kwa mujibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) jambo lililochangiwa na sera nzuri za fedha, utoshelevu wa chakula na kudhibiti bei za bidhaa zinazotoka nje.

Alifafanua kuwa mnamo Septemba 2024, Kampuni ya Kimataifa inayojihusisha na kufanya tathimini ya uwezo wa nchi kuyafikia masoko ya fedha ya kimataifa ya Moody's Investors Limited, imepandisha daraja la Tanzania kutoka B2 hadi B1.

*Uboreshaji hadi B1 unaonyesha rekodi ya Tanzania ya ustahimilivu wa uchumi ambayo inaruhusu Tanzania kupata kutambuliwa katika masoko ya fedha na mitaji ya kimataifa, na hivyo kuwezesha kuongezeka fursa za uwekezaji na upatikanaji mkubwa wa rasilimali fedha kwa sekta ya umma na binafsi," alifafanua Bi. Omolo.*



Mkurugenzi Mkuu Afrika wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bw. Naoki Yanase, akizungumza wakati wa mkutano na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, (hayupo pichani) uliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema kwa sasa Tanzania inaendelea kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na kubainisha kuwa ana tumaini Serikali ya Japani kupitia JICA itasaidia Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 ambayo inaandaliwa.

Kwa upande wake Bw. Naoki Yanase, Mkurugenzi Mkuu Afrika wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), alisema kuwa Japan itaendelea kushirikiana na Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuendeleza rasilimali watu kupitia ufadhili wa masomo.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo (wapili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu Afrika wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Bw. Naoki Yanase (wapili kushoto), pamoja na wajumbe wengine wa mkutano kati ya Wizara ya Fedha na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), uliyofanyika jijini Dodoma.

# BENKI YA DUNIA YAIPONGEZA TANZANIA MRADI WA SGR

*Na. Benny Mwaipaja*

Benki ya Dunia imeshangazwa na hatua kubwa iliyofikiwa na Serikali katika kutekeleza Mradi wa Kimkakati wa Reli ya Kisasa wa SGR, na kuahidi kuwa itaweka mkono wake kusaidia ujenzi wa Reli hiyo muhimu kwa kukuza biashara na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilitolewa Jijini Dar es Salaam, na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Benki ya Dunia anayesimamia Ujenzi wa Miundombinu, Bi. Wendy Hughes, alipokutana na kufanya mazungumzo na Mawaziri watatu wa Kisekta, wakiongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa na Waziri wa Ujenzi Mhe. Dkt. Abdallah Ulega.

Bi. Hughes aliyeambatana na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bw. Nathan Belete na Viongozi wengine waandamizi wa Benki hiyo, alisema kuwa amesafiri kwa kutumia reli hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na kushangazwa na kiwango cha ubora wake wa viwango vya kimataifa.







*Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akisalimiana na Mkurugenzi anayesimamaia Kanda ya Afrika wa Benki ya Dunia, Bi. Wendy Hughes, walipokutana na kufanya mazungumzo katika hoteli ya Rotana jijini Dar es Salaam.*

Alisema kuwa Benki ya Dunia inaendelea kuchakata maombi yaliyowasilishwa na Serikali katika Benki hiyo, na kwamba iko tayari kusaidia ujenzi wa Reli hiyo ya Kimkakati na kushauri pia sekta binafsi ishirikishwe kikamilifu kuhakikisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwa mradi huo yanafikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Wakizungumza katika kikao hicho kuhusu Mradi wa SGR, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, na Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Profesa Makame Mbarawa, waliishukuru Benki ya Dunia kwa kuamua kutoa fedha za kujenga mradi huo ambao umefikia hatua mbalimbali za ujenzi na ni mfano Barani Afrika na Duniani kwa ujumla.

Walieleza kuwa Mradi wa SGR unaogharimu zaidi ya shilingi trilioni 10 za Tanzania, ni muhimu katika kuimarisha biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo si tu kwa Tanzania, bali katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, ambapo biashara kati ya nchi hizo inatarajiwa kuongezeka na kusaidia kutatua tatizo la ajira kwa wananchi.

Mkutano huo uliowashirikisha Wakuu wa Taasisi katika Sekta ya Usafirishaji na Ujenzi, ulikuwa na ajenda tatu ikiwemo ujenzi wa Mradi wa Mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam-BRT, Mradi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa-SGR na namna ya kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza miradi kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi-PPP.

Tunakwenda Kidigitali kwa

# Kurahisisha Malipo Serikalini kupitia MUSE



# KONA YA MIKUTANO YA MWAKA YA IMF NA BENKI YA DUNIA 2024

NA BENNY MWAIPAJA





# DKT. NATU MWAMBA ASHIRIKI MJADALA KUHUSU UWEKEZAJI FEDHA KUKABILIANA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, ashiriki Mjadala kuhusu wajibu wa Benki Kuu za nchi za Afrika kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 30 tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Macroeconomic and Financial Management of Eastern and Southern Africa (MEFMI), mjadala uliofanyika kando ya Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), katika Hoteli ya Mayflower, Jijini Washington D.C, nchini Marekani.



Tukio hilo liliwakutanisha Mawaziri wa Fedha, Makatibu Wakuu na Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi za Afrika, ambapo kwa upande wa Tanzania. Walioshiriki, mbali na Dkt. Mwamba, ni Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Sera za Uchumi kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba.



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, wakiwa katika picha na Waziri wa Fedha na Maendeleo wa Lesotho, Dkt. Retselisitsoe Adelaide Matlanyane (Mb), baada ya mjadala kuhusu wajibu wa Benki Kuu za nchi za Afrika kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, mjadala uliofanyika kando ya Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), katika Hoteli ya Mayflower, Jijini Washington D.C, nchini Marekani.*



# IMF YAIMWAGIA SIFA TANZANIA KWA KUSIMAMIA UCHUMI WAKE KWA UMAHILI MKUBWA

Shirika la Fedha la Kimataifa, IMF, limeimwagia sifa Tanzania kwa namna inavyosimamia sera zake za uchumi na fedha ikiwemo kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa IMF anayesimamia Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika, Bw. Willie Nakunyanda, alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Tanzania ulioshiriki Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia, ulioongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Makao Makuu ya Taasisi hiyo, Jijini Washington D.C, nchini Marekani.

Kiongozi huyo alisema kuwa nchi nyingine za Afrika zinalo la kujifunza kuhusu usimamizi wa uchumi na sera za fedha kutoka Tanzania kutokana na umahili wake katika eneo hilo ambapo nchi imekuwa imara kiuchumi licha ya misukosuko mingi ya kiuchumi na kijamii inayojitokeza duniani.

Aliahidi kuwa Shirika la Fedha la Kimataifa-IFM litaendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania za kufanya mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Akizungumza katika Mkutano huo, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alisema kuwa Tanzania imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei ambao umebaki katika wigo wa tarakimu moja wa asilimia tatu.

Aidha, Dkt. Nchemba alisema kuwa sekeseke la uhaba wa dola za Marekani limedhibitiwa ambapo upatikanaji wa fedha za kigeni umekuwa tulivu huku benki zikiwa na akiba ya kutosha ya dola za Marekani ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

Dkt. Nchemba aliishukuru IMF kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi kupitia misaada, mikopo nafuu na misaada ya kiufundi Pamoja na miongozo mbalimbali inayoipatia nchi hatua iliyosaidia kuimarisha uchumi wa nchi.

Tanzania ni mwana hisa wa Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia na ushiriki wake katika Mikutano hiyo unalenga kulinda na kutetea maslahi ya nchi katika mashirika hayo makubwa ya fedha duniani kwa kushiriki mikutano ya kiutawala na uendeshaji.

Ujumbe wa Tanzania katika Mikutano hiyo umewashirikisha Magavana wa Taasisi hizo wakiongozwa na Mhe. Dkt. Nchemba, ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba.




# DKT. NCHEMBA AHIMIZA UIMARISHAJI WA NISHATI NCHI ZA AFRIKA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amezihimiza nchi za Afrika kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha Duniani pamoja na Sekta Binafsi, kuhakikisha kuwa zinawekeza kwenye uzalishaji wa nishati ya uhakika na yenye gharama nafuu ili kutimiza malengo ya kujiimarisha kiuchumi, kuchochea uwekezaji, uzalishaji wa bidhaa na huduma na kukuza ajira.

Dkt. Nchemba aliyasema hayo Jijini Washington D.C, nchini Marekani, wakati akishiriki mjadala kuhusu kuiwezesha Afrika kuwa na nishati ya uhakika, ulioandaliwa na Taasisi ya Mission 300, Kando ya Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia.

Dkt. Nchemba amesisitiza kuwa ushirikishwaji wa makundi mbalimbali katika kuzalisha nishati ikiwemo sekta binafsi, utachochea maendeleo katika Bara la Afrika kwa kuzalisha umeme wa kutosha na pia kufanyabiashara ya kuuziana umeme.



Alisema kuwa Tanzania kwa upande wake, kwa kushirikiana na mradi wa Benki ya Dunia wa kusaidia upatikanaji wa umeme wenye thamani yad ola za Marekani milioni 300, vijiji 11,837 vimeunganishwa na umeme na kuchochea maendeleo ya watu katika maeneo ya vijijini.

Aidha, alisema kuwa utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme nchini, unakwenda sambamba na hamasa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuweka sera, mipango, mikakati na kanuni zitakazochochea matumizi ya nishati hiyo safi ya kupikia.






Dkt. Nchemba alitumia fursa hiyo kuwakaribisha wadau wa maendeleo na Mawaziri wa Fedha wa nchi za Afrika kuwashawishi Wakuu wa nchi zao kushiriki Kilele cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu Nishati unaotarajiwa kufanyika Jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa mwezi januari mwaka 2025.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika AfDB anayesimamia masuala ya Nishati, Dkt. Kevin Kariuki, alisema kuwa Taasisi ya Mission 300 inajukumu la kuhakikisha kuwa suala la nishati linapewa kipaumbele katika mipango na sera za nchi za Afrika kutokana na umuhiku wake katika kukuza uchumi, usalama na kuharakisha maendeleo ya watu.

Alifafanua kuwa Mkutano wa Kilele wa Nishati utakaowashirikisha Wakuu wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, utaweka mikakati na uwezeshaji kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme.

Inakadiriwa kuwa Watu zaidi ya milioni 300 wanatarajiwa kuwa watakuwa wameunganishwa na umeme katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ifikapo Mwaka 2030, ikiwa ni jitihada za pamoja za wadau zikiwemo Taasisi za Fedha za Kimataifa na Sekta Binafsi kufanikisha mradi huo.





# MTANZANIA ACHAGULIWA KUWA MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA DUNIA

Benki ya Dunia, imemchagua Mtanzania, Dkt. Zarau Wendeline Kibwe, kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Benki hiyo atakayesimamia Kanda Namba Moja ya Afrika inayojumuisha nchi 22 ikiwemo Tanzania, nafasi ambayo Tanzania imewahi kuihudumu miaka 54 iliyopita.

Uamuzi wa Dkt. Kibwe kuikwaa nafasi hiyo nyeti katika Taasisi hiyo kubwa ya Fedha Duniani, ulitangazwa katika Mkutano wa Mwaka wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Benki ya Dunia, uliofanyika Jijini Washington D.C, nchini Marekani ambapo Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha Duniani IMF na Benki ya Dunia inafanyika.

Kabla ya kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Benki hiyo atakayesimamia Kanda Namba Moja ya Afrika, Dkt. Kibwe alihudumu katika Ofisi hiyo ya Bodi kama Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Mshauri na Mshauri Mwandamizi kwa zaidi ya miaka saba, tangu mwaka 2017.

Akizungumza Jijini Washington D.C, baada ya kutangazwa kuchukua nafasi hiyo, Dkt. Zarau Wendeline Kibwe alisema kuwa ataitumia nafasi hiyo kusimamia uendeshaji wa Benki na Taasisi zake Pamoja na kutetea Maslahi ya nchi katika Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia pamoja na maslahi ya Kanda ya Afrika anayoisimamia ili kukuza maendeleo na uchumi wa nchi hizo.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali katika Mkutano huo uliomtangaza Dk. Kibwe kuchukua nafasi hiyo, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alisema kuwa hayo ni matokeo ya juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anavyoifungua nchi na kukuza Diplomasia ya Kimataifa.

Dkt. Nchemba alimpongeza Dkt. Kibwe kwa kupata nafasi hiyo na kwamba kutokana na umahili wake katika masuala ya uchumi na fedha, pamoja na uzoefu wake wa muda mrefu katika Ofisi hiyo, anaamini kuwa maslahi ya nchi yataendelea kulindwa ipasavyo kwa manufaa ya watanzania.



Dkt. Zarau Wendeline Kibwe ni mchumi wa kitanzania ambaye hivi karibuni amechaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia kwa Kanda Namba Moja ya Afrika inayojumuisha nchi za Botswana, Burundi, Eritrea, Eswatini, Ethiopia, Gambia, Kenya, Lesotho, Liberia, Malawi, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Shelisheli, Sierra Leone, Somalia, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

Kabla ya kujiunga na Ofisi ya Bodi, Dkt Kibwe alihudumu kama Mchumi wa Benki ya Dunia kwa Tanzania ambapo katika kipindi cha miaka 15 ya kazi yake, Dkt. Kibwe amehudumu katika Serikali ya Jamhuri wa Muungano katika nafasi mbalimbali ikiwemo ya Mchambuzi Mwanadamizi wa Sera (Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango), Mhadhiri Msaidizi (Chuo Kikuu Dodoma), Afisa Forodha Msaidizi (Mamlaka ya Mapato Tanzania), na Mhadhiri Msaidizi (Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere).

Dkt. Kibwe ana Shahada ya Uzamivu (Ph.D.) katika Uchumi wa Maendeleo, Shahada ya Uzamili (MA) katika Uchumi wa Maendeleo, na Shahada ya Umahiri katika Sera za Umma, zote kutoka Taasisi ya Taifa ya Mafunzo ya Sera (GRIPS) huko Tokyo, Japani.

Alipata Shahada yake ya Kwanza ya Sayansi katika Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe kilichopo Morogoro, Tanzania.



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (katikati), akiwa na Viongozi wengine, Waziri wa Fedha wa Burundi, Mhe. Audace Niyonzima (wa tatu kulia), Waziri wa Fedha na Mipango-Zanzibar, Dkt. Saada Mkuya Salum (wa tatu kushoto, Balozi wa Tanzania-Marekani, Mhe. Dkt. Elsie Kanza (kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha- Dkt. Natu El-maamry Mwamba (wa pili kulia), Mkurugenzi Mtendaji anayesimamia Kanda Namba Moja ya Afrika, aliyemaliza muda wake, Dkt. Floribert Ngaruko (kulia) akiwa katika picha na Mkurugenzi Mtendaji Mpya wa Kundi hilo la Kanda namba Moja ya Afrika ya Benki ya Dunia kutoka Tanzania, Dkt. Zarau Wendeline Kibwe (wa pili kushoto), baada ya kutangazwa rasmi katika Mkutano wa Mwaka wa Kanda hiyo kushika wadhifa huo, Jijini Washington D.C, nchini Marekani.*






# DKT. NCHEMBA ASHIRIKI MKUTANO WA MAGAVANA WA BENKI YA DUNIA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), ameshiriki Mkutano wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu za nchi za Afrika (African Caucus - WB) uliomshirikisha Rais wa Benki ya Dunia, Bw. Ajay Banga, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambako Dkt. Nchemba, aliongoza Ujumbe wa Tanzania katika Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia.

Mkutano huo uliwapa fursa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu za Afrika kuwasilisha vipaumbele na changamoto zinazoathiri maendeleo barani Afrika kwa Rais wa Benki ya Dunia Bw. Ajay Banga, ili kuzingatiwa katika mipango na mikakati ya ushirikiano kati ya Benki ya Dunia na nchi za Afrika. Baadhi ya changamoto zilizoainishwa ni pamoja na: fursa chache za ajira kwa vijana; miundombinu hafifu ya umeme, barabara na tehama; uzalishaji mdogo wa chakula; tishio katika uhimilivu wa madeni; na ongezeko la gharama za upatikanaji wa mikopo.

Bw. Banga alikubaliana na umuhimu wa upatikanaji wa umeme wa uhakika na wakutosha katika kuchochea shughuli za uchumi na namna unavyoweza kuathiri uzalishaji wa mbolea na chakula. Hivyo alibainisha kuwa Benki ya Dunia ipo tayari kusaidia utekelezaji wa miradi ya umeme ambayo inahusisha matumizi ya nishati rafiki kwa mazingira na kuhimiza matumizi ya TEHAMA hususan kwa kundi kubwa la vijana kwa kuwa ni chanzo moja wapo kikubwa cha ajira.




*Rais wa Benki ya Dunia, Bw. Ajay Banga, akizungumza wakati wa Mkutano wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu za Nchi za Afrika (African Caucus-WB), uliofanyika jijini Washington D.C nchini Marekani.*




# DKT. NCHEMBA ATETA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA IDFC NCHINI MAREKANI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (International Development Finance Corporation), Bw. Scott Nathan, ambapo wamejadili kuhusu ushirikianao kati ya Tanzania na Shirika hilo katika sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo madini, ukuzaji biashara ndogondogo na kuisaidia sekta binafsi ili kuharakisha maendeleo ya nchi.

Mkutano huo ulifanyika kando ya Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia Jijini Washington D.C, nchini Marekani.







# DKT. NCHEMBA AHIMIZA MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MIKUTANO YA BENKI YA DUNIA NA IMF

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amerejea wito wa Tanzania kwa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kukifanya Kiswahili kuwa miongozi mwa lugha rasmi za mawasiliano katika mikutano ya Taasisi hizo kubwa za Fedha Duniani.

Dkt. Nchemba alitoa rai hiyo alipoongoza Ujumbe wa Tanzania katika mazungumzo na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambako Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF na Benki ya Dunia inafanyika.

Alisisitiza kuwa Kiswahili ni lugha ya Afrika na pia ni lugha rasmi inayotumika katika Mikutano ya Umoja wa Afrika hivyo imefika wakati kwa Taasisi hizo kubwa za Fedha Duniani kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha zinazotambulika rasmi na kutumika katika Mikutano ya Benki ya Dunia na IMF.

Katika hatua nyingine, Dkt. Nchemba aliishukuru pia Benki ya Dunia kwa kuahidi kusaidia ujenzi wa mradi mkubwa wa Reli ya Kisasa SGR, unaoendelea nchini Tanzania kwa kuwa mradi huo ni miongozi mwa miradi ya kipaumbele ya kitaifa kutokana na umuhimu wake katika kukuza biashara na uchumi wa nchi na mataifa mengine yatakayounganishwa na Reli hiyo.

Aidha, Dkt. Nchemba, alitoa shukrani kwa uamuzi wa Benki ya Dunia, kubeba ajenda ya kuwawezesha na kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili waweze kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa nchini Tanzania kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia na IMF badala ya mfumo wa sasa unaowanufaisha zaidi wakandarasi wa kigeni.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki, Bi. Victoria Kwakwa, aliahidi kuwa Benki ya Dunia itaendelea kushirikiana na Tanzania kwa kuiwezesha kutimiza malengo yake ya kimaendeleo na kiuchumi kupitia misaada ya kiufundi na kifedha.

Bi. Kwakwa alieleza kuwa mradi wa Reli ya Kisasa wa SGR, mradi wa kusambaza nishati ya umeme hususan vijijini, kuwawezesha wakandarasi kupata zabuni za miradi na mradi wa kuboresha elimu ni miongoni mwa mipango itakayopewa kipaumbele ili kuharakisha maendeleo ya watu na kuimarisha uchumi wa Tanzania.

# KUTOKA MIKUTANO YA COP29

## NA BENNY MWAIPAJA



# DKT. NCHEMBA AHIMIZA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ametoa wito kwa Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa maendeleo kuunga mkono agenda ya kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa manufaa ya watu waishio Barani Afrika.

Dkt. Nchemba alitoa wito huo wakati akifunga mkutano uliojadili umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeongoza Ujumbe wa Tanzania katika Mikutano hiyo,  Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Alisema kuwa ni muhimu kwa nchi za Afrika kutekeleza sera zinazochochea kasi ya matumizi ya teknolojia za nishati safi ya kupikia na kutenga fedha za kutosha kuisadia jamii hususan iliyoathirika zaidi na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi.



*Ni muhimu kujenga ushirikiano unaolenga kuongeza ujuzi na utaalam ili kuhakikisha kuwa suluhisho la changamoto ya matumizi duni ya teknolojia ya kuwezesha matumizi ya nishati safi ya kupikia inapatiwa ufumbuzi wa kudumu" alisema Dkt. Nchemba kwa niaba ya Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mpango*

Dkt. Nchemba alisisitiza umuhimu wa wadau wote kushirikiana ili kuweka mazingira wezeshi ya mipango ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kujenga mustakabari na kesho iliyobora kote Barani Afrika.




Mkutano huo wa nishati safi ya kupikia uliandaliwa na Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU) pamoja na Tume ya Nishati Afrika (AFREC) uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Zaidi wa watu elfu 50, wakiwemo wanadiplomasia kutoka zaidi ya nchi 200 wanachama wa Umoja wa Mataifa, walikutana katika Jiji la Baku, nchini Azerbaijan, walijadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutafuta vyanzo vya fedha za uhakika za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwemo kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# DKT. NCHEMBA AJADILI UPATIKANAJI FEDHA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amezitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi yao ya kutoa dola za marekani bilioni 500, sawa na dola bilioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi katika kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2025.

Mhe. Dkt. Nchemba (Mb), alitoa kauli hiyo wakati akichangia hoja katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Mawaziri uliojadili namna ya kupata fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Alisema kuwa ripoti ya Mkutano wa COP28, uliofanyika Dubai mwaka 2023, inaonesha kwamba kuna kasi ndogo katika kutimiza ahadi ya Mkataba wa Paris katika kuhamasisha upatikanaji ama uchangiaji wa dola 100 bilioni ambapo kuna pengo la takribani dola bilioni 60 kila mwaka hali inayo ziathiri nchi zinazoendelea katika kupanga mipango ya maendeleo.

Aidha, Dkt. Nchemba alisema kuwa Tanzania inataka kuwe na uwazi katika namna fedha hizo dola bilioni 100 zinazotakiwa kutolewa kila mwaka kwa nchi zinzoendelea ili kuweka uwajibikaji kulingana na Mkataba wa Paris kuhusu suala hilo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa mabadiliko ya Tabianchi ni janga linalobomoa Uchumi wa nchi zinazoendelea na kushauri




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akishiriki Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Mawaziri uliojadili namna ya kupata fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku nchini Azerbaijan.*

matamanio na ahadi zinazotolewa na mataifa makubwa yawekwe katika vitendo ili kuzinusuru nchi zinazoendelea kutokana na madhara yanayosababishwa na mabadiliko hayo ya tabianchi.

Dkt. Nchemba alisema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea iliyoathirika na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi na inajitahidi kutumia rasilimali zake kukabiliana na athari hizo ikiwemo kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko lakini fedha hizo za ndani hazitoshelezi mahitaji.

*Pia tunatoa wito wa kupitia upya usanifu wa kifedha wa kimataifa na utaratibu wa ufadhili chini ya mkataba ili kusaidia uhamasishaji wa fedha thabiti na za muda mrefu kwa kiwango cha uwekezaji unaohitajika na nchi zinazoendelea kupambana na shida ya mabadiliko ya tabianchi" Alisisitiza Mhe. Dkt. Nchemba*






# MAKAMU WA RAIS ANADI FURSA ZA UWEKEZAJI SEKTA YA UCHUMI WA BULUU




Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, ameihamasisha sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo wa kimataifa kuchangamkia fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini Tanzania katika sekta ya uchumi wa buluu kwa faida za kiuchumi na hifadhi ya mazingira ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Dkt. Mpango alitoa wito huo katika Hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Ashatu Kijaji, wakati akifungua mkutano wa kunadi fursa za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu zilizopo Tanzania, uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Mkutano huo wa kunadi fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uchumi wa Buluu uliandaliwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania na Wizara ya Uchumi wa Buluu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi kutoka Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Hifadhi ya Maliasili (IUCN) na mashirika mengineyo.

Dkt. Kijaji alisema kuwa kuwekeza katika shughuli endelevu za uchumi wa bluu na miradi ya kurejesha, kama vile marejesho ya mikoko, miamba ya matumbawe na Bahari, uhifadhi wa maeneo ya mvua na kilimo cha mwani kinaweza kuongeza utenganishaji wa kaboni na kusaidia malengo ya kukabiliana na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya Kyoto na Mkataba wa Paris.

Aliyataja maeneo ya uwekezaji kuwa ni pamoja na uchimbaji wa madini, uvunaji wa mafuta na gesi, ujenzi wa bandari kavu, uvuvi mkubwa katika kina cha Bahari katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 223,000.

Alisema kwamba uwekezaji huo utachangia kukuza uchumi wa nchi na wawekezaji, lakini pia utakuza ajira kwa makundi ya watu wanaojihusisha na shughuli mbalimbali baharini na vyanzo vingine vya maji.

Dkt. Kijaji alibainisha kuwa Tanzania imeendelea kujenga miundombinu wezeshi ya kurahisisha ufanyajikazi katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwemo kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya Bahari ili kuyaongezea thamani ikiwemo zao la mwani na



kujenga viwanja vya ndege na bandari Visiwani Zanzibar na mikoa ya Kusini.

Wakizungumza katika mkutano huo, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Zanzibar, Bw. Zahor Kassim El Kharousy, walieleza umuhimu wa uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwemo upatikanaji wa kodi pamoja na maendeleo ya watu.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano wa Mazingira), Dkt. Ashatu Kijaji, akifungua Mkutano wa Kunadi fursa za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu zilizopo Tanzania kwa niaba ya Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.*

Zaidi ya watu 200 toka mataifa mbalimbali wakiwemo viongozi waandamizi kutoka Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Hifadhi ya Maliasili (IUCN) na mashirika mengineyo ambapo waliahidi kuendelea kusaidiana na Tanzania kwenye upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya masuala ya kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya Tabia nchi kwenye sekta ya Uvuvi nchini Tanzania.




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akizungumza wakati wa Mkutano wa Kunadi fursa za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu zilizopo Tanzania, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) uliofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.*



# Kamera Yetu



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akiteta jambo na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), katika Banda la Maonesho la Tanzania, katika Uwanja wa Michezo wa Baku, ulipofanyika Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29), Jijini Baku nchini Azerbaijan, ambapo Mhe. Makamu wa Rais aliongoza Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.*




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Mahmood Thabit Kombo (Mb) wakifurahia jambo baada ya kushiriki Mkutano wa Dharura wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika kwa njia ya mtandao kutokea Ofisi Ndogo za Wizara ya Mambo ya Nje, Jijini Dar es Salaam, ambapo ajenda kuu ilikuwa kujadili ulinzi wa amani.*



*Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (kushoto), akiagana na Kiongozi wa Timu ya Wataalamu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Charalambos Tsangarides, baada ya kutamatika kwa kikao chao cha kuhitimisha tathmini ya Awamu ya Nne ya utekelezaji wa Program ya Extended Credit Facility-(ECF), inayohusisha upatikanaji wa mkopo nafuu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na huduma za jamii pamoja na kufanya mapitio na tathmini ya kwanza (1st Review) ya Program mpya ya Serikali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia Dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF), jijini Dar es Salaam.*



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), Katikati), Naibu Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Mhe. Axel-David Guuillon (kulia) na  Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Bi. Celine Robert, wakionesha Hati za Mikataba yenye jumla ya euro milioni 118.8 sawa na takriban shilingi bilioni 323.4 zilizotolewa na AFD, kwa ajili kutekeleza miradi mbalimbali nchini ikiwemo Awamu ya Pili ya Mradi wa Nishati-jua wa Kishapu Mkoani Shinyanga pamoja na uendelezaji wa misitu na utunzaji wa Hifadhi ya Misitu ya Mikoko, Jijini Dar es Salaam.



Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja, akimkabidhi Tuzo, Afisa Utafiti na Mawasiliano wa Umoja wa Mabenki (Tanzania Bankers Assosication – TBA), Bi. Sophia Mmbuji baada ya TBA kuibuka mshindi wa uhamasishaji bora wa maadhimisho katika vyama vilele kwa uratibu wa taasisi zao na kufanikisha ushiriki kwa zaidi ya asilimia 50, wakati wa hafla ya kufunga Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, yenye kaulimbiu “Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi”, yaliyofanyika katika Viwanja vya Ruanda-Nzovwe, Jijini Mbeya, ambayo yalizikutanisha Taasisi Ndogo za Fedha, Benki, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na wajasiriamali kutoka mkoa wa Mbeya na mikoa jirani.




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akizindua rasmi utoaji wa Hati Fungani ijulikanayo kama “Bondi Yangu” ya Benki ya Azania, inayotarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 100 kupitia soko la mitaji, hatua ambayo amesema ni kielelezo tosha cha umuhimu uliowekwa na Benki hiyo katika kukuza Sekta ya Fedha nchini, Tukio lililofanyika katika Hoteli ya Best Western, Jijini Dodoma.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba (wa pili kulia), Mkuu wa Masuala ya Ushirikiano wa Umoja wa Ulaya (EU), Bw. Marc Stalmans (wa kwanza kulia) na Naibu Gavana wa Benki kuu ya Tanzania, Bi. Sauda Msemo (wa pili kushoto), wakiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa kikao cha Majadiliano kati ya wataalamu wa Serikali na Umoja wa Ulaya, kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali ya Tanzania (Budget Support dialogue meeting for the Finance for Growth Programme)



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El – Maamry Mwamba, (katikati), Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Mhe. Susan Namondo (kushoto) na Naibu Balozi wa Ireland Tanzania, Mhe. Mags Gaynor, wakiwa katika picha ya pamoja na ujumbe wa Serikali na Wadau wa Maendeleo baada ya kuzindua Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Coopera-tion Framework 2017/2018- 2024/2025)



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akifurahia jambo na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dkt. Akinwumi Adesina, katika Viwanja vya Michezo vya Olimpiki, Baku, nchini Azerbaijan, unapofanyika Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29).*



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Bi. Happiness Seneda (Kushoto), akioneshwa namna ya kupakua hati ya Mshahara (Salary Slip) katika mfumo wa Salary Slip Portal, kwa kutumia simu janja, na Afisa Tehama Mwandamizi, Wizara ya Fedha, Bi. Zaina Mwanga, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, yenye kaulimbiu "Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi", yaliyofanyika katika Viwanja vya Ruanda-Nzovwe, Jijini Mbeya, ambayo yalizikutanisha Taasisi Ndogo za Fedha, Benki, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na wajasiriamali kutoka mkoa wa Mbeya na mikoa jirani.*



*Waziri wa Fedha, Mhe, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), akiwa na Walimu wake waliomfundisha Masuala ya Uchumi na Fedha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, walipokutana ana kwa ana wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Kwanza la Wadau wa Sekta ya Fedha kwa mwaka 2024, katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akiagana na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, CGP Jeremiah Yoram Katungu, ambaye alifika ofisini kwake kujitambulisha na kuongelea mipango ya maendeleo ya Jeshi la Magereza, jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, akiagana na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Bw. Jean Francois Arnal, baada ya mkutano kati yao kuhusu ushirikiano kati ya Tanzania na Ufaransa, utekelezaji wa miradi ya nishati na kuainisha miradi mipya inayotarajiwa kutekelezwa kupitia Shirika hilo, jijini Dodoma.*



*Kamishna Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Madeni, Wizara ya Fedha, Bw. Omary Khama akiteta jambo na Mkuu wa Ushirikiano kutoka Ubalozi wa Finland, Bw. Juhana Lehtninen baada ya Semina ya Ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo nchini, jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa United Bank of Africa (UBA), Bw. Gbenga Makinde, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam, ambapo aliishukuru Benki hiyo kwa kuwa tayari kuendelea kushirikiana na Serikali katika kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo.*



*Mchumi Mkuu kutoka Idara ya Bajeti, Wizara ya Fedha, Bw. Cosmas Nshenye (Kushoto), akiwaelezea Wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole-Mbeya (CDTI), kuhusu namna Bajeti ya Serikali inavyoandaliwa, walipotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, yenye kaulimbiu "Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi", yaliyofanyika katika Viwanja vya Ruanda-Nzovwe, Jijini Mbeya, ambayo yalizikutanisha Taasisi Ndogo za Fedha, Benki, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na wajasiriamali kutoka mkoa wa Mbeya na mikoa jirani.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu lameck Nchemba Madelu (Mb), akiwa na Waziri wa Fedha wa Burundi, Mhe. Audace Niyonzima baada ya kufanya mazungumzo, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambapo mazungumzo yao yalilenga namna ya kupata fedha kutoka Benki ya Dunia na IMF, kwa ajili ya kujenga Reli ya Kisasa ya SGR itakayounganisha nchi hizo mbili kuanzia Uvinza-Msongati-Gitega - Uvira hadi Kindu nchini Burundi.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban (Katikati), akikabidhiwa tuzo ya shukrani na Rais wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania (IIA), Dkt. Zelia Njeza (Kushoto) kwa niaba ya Katibu Mkuu, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, kwa mchango wake katika kufanikisha Mkutano wa 10 wa Wakaguzi wa Ndani Barani Afrika na kusaidia ukuaji wa kada ya ukaguzi wa ndani, walipokutana na kufanya mazungumzo, katika Ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma. Kulia ni Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG), Bw. Benjamin Magai.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bi. Jenifa Christian Omolo (katikati), akiwa katika maandamano ya Mahafali ya 22 ya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) katika Kampasi ya Dar es Salaam Viwanja vya Kurasini ambayo ni Makao Makuu ya Taasisi hiyo. Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Prof. William Pallangyo na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Uhasibu Prof. Jehovaness Aikael.*

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA
MJI WA SERIKALI - MTUMBA
MTAA WA HAZINA
S.L.P 2802, 40468 DODOMA, TANZANIA
www.mof.go.tz